**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

## MHESHIMIWA MASOUD ALI MOHAMMED (MBM)

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**
**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI - ZANZIBAR**

**MEI, 2021**

## Yaliyomo


**UTANGULIZI** ..... 3

**MAFANIKIO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021** ..... 8

**UPATIKANAJI WA FEDHA** ..... 8

**PROGRAMU ZA MAKAO MAKUU (FUNGU D01)** ..... 11

**PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ** ..... 11

- PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA ORTMSMIM ..... 11
- PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA KAZI ZA MIPANGO, SERA NA UTAFITI ..... 12
- PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA ..... 13
- PROGRAMU NDOGO YA USAJILI NA URATIBU WA JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI (NGOs) ..... 14
- WAKALA WA ULINZI JKU ..... 15

**PROGRAMU KUU YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** ..... 15

- PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SERIKALI ZA MITAA ..... 16

**PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI NA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SMZ** ..... 17

- PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SMZ ..... 17
- PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA UTUMISHI WA IDARA MAALUM ZA SMZ ..... 18

**PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU D02-D06)** ..... 19

**JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) - FUNGU D02** ..... 19

**CHUO CHA MAFUNZO (MF) – FUNGU D03** ..... 22

**KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)- FUNGU D04** ..... 24

**KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) - FUNGU D05** ..... 25

**KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ) - FUNGU D06** ..... 27

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (FUNGU D07-D11)** ..... 29

**MKOA WA MJINI MAGHARIBI - FUNGU (D07)** ..... 29

**MKOA WA KUSINI UNGUJA – FUNGU (D08)** ..... 40

**MKOA WA KASKAZINI UNGUJA - (D09)** ..... 48

**MKOA WA KUSINI PEMBA – FUNGU (D10)** ..... 56

**MKOA WA KASKAZINI PEMBA - FUNGU D11** ..... 63

**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII – FUNGU D12** ..... 70

**MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022** ..... 71

**PROGRAMU ZA MAKAO MAKUU FUNGU-D01** ..... 72

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA OR - TMSMIM-SMZ** ..... 72

- PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA ORTMSMIM ..... 72
- PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA KAZI ZA MIPANGO, SERA NA UTAFITI ..... 73
- PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA OFISI PEMBA ..... 73
- PROGRAM NDOGO YA USAJILI NA URATIBU WA JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI ..... 74
- WAKALA WA ULINZI JKU ..... 74

**PROGRAMU KUU YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** ..... 75

PROGRAMU KUU YA URATIBU NA USIMAMIZI WA IDARA MAALUM ZA SMZ ........................ 76
PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA IDARA MAALUM ........................ 76
TUME YA UTUMISHI WA IDARA MAALUM ZA SMZ ........................ 76
PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ - FUNGU (D02-D06) ........................ 77
JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) - FUNGU D02 ........................ 77
CHUO CHA MAFUNZO - FUNGU D03 ........................ 78
KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) - FUNGU D04 ........................ 78
KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) - FUNGU D05 ........................ 79
KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ) – FUNGU D06 ........................ 80
KAMPUNI YA UJENZI YA SERIKALI ........................ 81
PROGRAMU ZA TAWALA ZA MIKOA - FUNGU (D07-D11) ........................ 81
MKOA WA MJINI MAGHARIBI – FUNGU D07 ........................ 82
MKOA WA KUSINI UNGUJA – FUNGU D08 ........................ 84
MKOA WA KASKAZINI UNGUJA – FUNGU D09 ........................ 85
MKOA WA KUSINI PEMBA – FUNGU D10 ........................ 87
MKOA WA KASKAZINI PEMBA – FUNGU D11 ........................ 88
WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII –FUNGU D12 ........................ 89
SHUKRANI ........................ 90
HITIMISHO ........................ 92

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa amani na utulivu pamoja na kuendeleza mshikamano na umoja wa kitaifa katika ujenzi wa maendeleo ya nchi yetu.
3. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na unyenyekevu mkubwa nampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kwa ushindi mkubwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 2020 na kuapishwa tarehe 02/11/2020.
4. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar na kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kusimamia shughuli za Serikali.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa misiba mikubwa iliyoikumba Taifa letu ya kuondokewa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Maalim Seif Sharif Hamad aliyekuwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Kuondoka kwao ni pigo kubwa si kwa Tanzania tu bali ni pigo kwa Afrika Mashariki, Bara la Afrika na Dunia nzima kwa ujumla kutokana na mchango mkubwa wa Viongozi hao katika Taifa hili.
6. **Mheshimiwa Spika,** nichukue nafasi hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia kauli mbiu yake ya "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi Iendelee", Wazanzibari na Watanzania tuna imani kuwa kazi inaendelea huku tukiamini Taifa litaendelea kupiga hatua kubwa ya maendeleo na tunaahidi kumpa ushirikiano wa hali ya juu katika kuhakikisha Taifa linafikia malengo yaliyojipangia.
7. **Mheshimiwa Spika,** kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Namuahidi Mheshimiwa Rais kuwa nitafanya kazi kwa bidii, weledi, uadilifu, ubunifu, uaminifu na utiifu kwake na kwa nchi yetu katika kumsaidia na kumshauri kwa mujibu wa kiapo changu wakati wa kuniapisha. Aidha, kwa kushirikiana na watendaji wenzangu, tutaongeza jitihada za kusimamia matumizi ya fedha za umma kwa Taasisi zote zilizo chini ya usimamizi wa Wizara hii.
8. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa nakupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwenu kuliongoza tena Baraza hili Tukufu kwa kipindi kingine cha awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kuchaguliwa kwenu kumeonesha ushahidi wa umahiri mkubwa mlionao katika kuliendesha Baraza hili Tukufu. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Baraza kwa kuchaguliwa kwao pamoja na viongozi wengine mbali mbali wa Baraza. Nawaombea wote Mungu awajaalie

uwezo na uongozi mahiri, wenye hekima, busara na uadilifu wa kutimiza majukumu yenu Barazani.

9. **Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wa pekee nampongeza Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh, Mwakilishi wa Wananchi, Jimbo la Welezo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf, Mwakilishi wa Wananchi, Jimbo la Bumbwini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii. Nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ambao ni Mheshimiwa Suleiman Makame Ali, Mheshimiwa Salma Mussa Bilal, Mheshimiwa Machano Othman Said, Mheshimiwa Zaina Abdalla Salum na Mheshimiwa Moh'd Mgaza Jecha bila ya kuwasahau Makatibu wa Kamati. Michango yao katika ziara walizozifanya katika taasisi za Wizara hii imesaidia kuimarisha utendaji. Aidha, Kamati imeweza kupitia bajeti na kupitisha mafungu yote kitendo ambacho kimetupa matumaini makubwa ya Kamati katika kutushauri.

10. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutaja majukumu ya Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mujibu wa muundo mpya katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Awamu ya nane kama ifuatayo:-

i. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Sekta;
ii. Kufanya na kukuza tafiti zinazohusiana na maendeleo ya Sekta;
iii. Kusimamia uongozi wa rasilimali watu, fedha na rasilimali nyenginezo;
iv. Kusimamia na kuratibu majukumu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
v. Kusimamia Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar;
vi. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa majukumu ya Idara Maalum za SMZ;
vii. Kusimamia na kuweka utaratibu wa huduma za kiulinzi kwa taasisi za umma na taasisi binafsi;
viii. Kusimamia na kuratibu shughuli za Jumuiya zisizo za kiserikali;
ix. Kusikiliza malalamiko ya wananchi na kuyapatia ufumbuzi.

**Mheshimiwa Spika,** nitumie nafasi hii sasa kuorodhesha Dira, Dhamira na Programu Kuu zinazotekelezwa na Wizara hii kama ifuatavyo:-

**DIRA**

Kuwa taasisi imara katika kusimamia amani, usalama, usajili wa wakaazi na upatikanaji wa huduma karibu na wananchi.

**DHAMIRA**

Kujenga mazingira mazuri ya ushiriki wa wananchi katika kudumisha amani, ulinzi wa mali zao, kuimarisha huduma za kijamii, kuhakikisha kuwa jamii inashiriki katika kupanga na kusimamia shughuli za maendeleo katika maeneo yao kwa kuzingatia misingi ya utawala bora ikihusisha kuwatambua wakaazi wa maeneo husika na utambulisho wao.

**PROGRAMU ZINAZOTEKELEZWA NA AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ**

**PROGRAMU ZA OFISI KUU (FUNGU D01)**

1. Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
2. Programu ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
3. Programu ya Usimamizi wa Utumishi na Uratibu wa Idara Maalum za SMZ.

**PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU D02-D06)**

1. Programu ya Mafunzo kwa Vijana na Uzalishajimali ya JKU
2. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa JKU
3. Programu ya Urekebishaji Tabia kwa Wanafunzi ya Chuo cha Mafunzo
4. Programu ya Uongozi na Utawala wa Chuo Cha Mafunzo
5. Programu ya Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo ya KMKM
6. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa huduma za KMKM
7. Programu ya Uzimaji moto na Uokozi
8. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi
9. Programu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao

10. Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Kikosi cha Valantia Zanzibar

**PROGRAMU ZA TAWALA ZA MIKOA (FUNGU D07-D11)**

1. Programu ya Kusimamia Shughuli za Serikali katika Mkoa
2. Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa Tawala za Mikoa
3. Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa

**PROGRAMU ZA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII (FUNGU D12)**

1. Programu ya Usajili wa Matukio ya Kijamii
2. Programu ya Utumishi na Uendeshaji.

11. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, sasa naomba uniruhusu niwasilishe utekelezaji wa Programu za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2020/2021.

12. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inatekeleza majukumu yake kupitia programu kubwa 18. Programu hizo zimegawanyika katika mafungu D01 hadi D12. Fungu D01 ni Programu zinazotekelezwa na Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu, Mafungu D02 hadi D06 yanahusu Idara Maalum za SMZ, Mafungu D07 hadi D11 ni Programu za Mikoa na Fungu D12 ni Programu za Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii. Kutokana na mafungu haya ya kibajeti mafanikio yafuatayo yamepatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021;

**13.**

**MAFANIKIO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**14.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ujumla imepata mafanikio yafuatayo;

i. Kuimarika ulinzi, usalama, amani, utulivu na mshikamano wa Kitaifa wakati wa Uchaguzi Mkuu na baada ya Uchaguzi Mkuu kupitia Idara Maalum za SMZ na Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya;

ii. Kuimarika mahusiano baina ya Serikali na Wananchi kufuatia ziara zinazofanywa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi kwa mashirikiano na Sekta husika;

iii. Kuwa kiungo muhimu cha mapambano dhidi ya udhalilishaji wa watoto na unyanyasaji wa kijinsia ambapo Afisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya zimekuwa mstari wa mbele kufuatilia, kufichua na kuelimisha jamii;

iv. Kupungua kwa majanga ya moto na athari zake kutokana na kazi nzuri inayofanywa na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kwa kufika kwenye matukio yanayojitokeza kwa wakati na mpango wake wa kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari juu ya tahadhari za kuchukua;

v. Kuimarika kwa makaazi na mazingira ya kazi katika Kambi za Idara Maalum za SMZ kupitia Mradi ulioanzishwa na Serikali wa kujenga mahanga, nyumba za maafisa na majengo kwa ujumla;

vi. Kuimarika uwajibikaji wa Jumuiya zisizo za Kiserikali katika kutekeleza shughuli zao na kuondokana na Jumuiya ambazo zilikuwepo kwa maslahi binafsi;

vii. Kupunguza vitendo vya rushwa, ubadhirifu na matumizi mabaya ya rasilimali fedha, rasilimali watu na mali za Serikali.

**UPATIKANAJI WA FEDHA**

**15.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 252,697,370,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi**

**103,500,900,000** mishahara, **Shilingi 35,275,860,000** matumizi mengineyo, **Shilingi 83,024,380,000** ruzuku kwa Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ, Wakala wa Ulinzi JKU na Mamlaka za Serikali za Mitaa na **Shilingi 30,896,230,000** kwa kazi za maendeleo ikijumuisha **Shilingi 2,896,230,000** mchango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2021, Ofisi iliingiziwa **Shilingi 157,796,233,191** sawa na asilimia **62** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 81,177,345,776** sawa na asilimia **78** ni mishahara, **Shilingi 15,498,219,306** sawa na asilimia **44** matumizi mengineyo, **Shilingi 52,528,991,921** sawa na asilimia **63** ni ruzuku kwa Tume ya Utumishi ya Idara Maalum, Wakala wa Ulinzi JKU na Mamlaka za Serikali za Mitaa na **Shilingi 12,758,802,098** sawa na asilimia **46** kwa kazi za maendeleo. **(Angalia kiambatisho namba 1, 2 a na 2 b).**

16. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mapato, Ofisi iliidhinishiwa kukusanya **Shilingi 1,990,724,000** kwa ajili ya kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina na kukusanya **Shilingi 971,949,460** sawa na asilimia **69** ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa kukusanya **Shilingi 15,240,271,665** na kukusanya **Shilingi 10,534,774,108** sawa na asilimia **69** ya makadirio ya mwaka. **(Angalia kiambatisho namba 3a na 3b).**

**UTEKELEZAJI WA JUMLA**

17. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Afisi imeratibu na kusimamia uajiri wa watumishi wapya kwa taasisi zilizochini ya usimamizi wa Wizara. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya watumishi wapya 478 wameajiriwa katika kada mbalimbali kama inavyoonekana katika ***kiambatisho namba 4a.*** Aidha, kupitia Mafungu yote yaliyoanzia D01 hadi D12, jumla ya watendaji 114 wamejengewa uwezo kupitia mafunzo ya muda mrefu katika ngazi na fani mbali mbali ambapo wanawake ni 46 na wanaume 68 ***(Angalia kiambatisho namba 4b)***. Vile vile, kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, jumla ya wakulima 24,934, Wafugaji 9,814 na Wavuvi 4,257 wamepatiwa elimu ya udhibiti wa magonjwa ya mifugo na mazao na

elimu ya kuongeza kiwango cha uzalishaji kama inavyoonekana katika ***kiambatisho namba 11.***

**18.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha huduma za afya kwa wananchi, jitihada mbali mbali zimeendelea kufanyika ikiwemo utoaji wa huduma za mama na mtoto, utoaji wa chanjo, utoaji wa elimu ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza na ugawaji wa dawa na vifaa tiba. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2020/2021, jumla ya wagonjwa 2,335,011 wamehudhuria katika vituo vya afya na kupatiwa huduma. Kati ya hao wanawake 1,366,283 na wanaume 968,728 ***(Angalia kiambatisho namba 5).***

**19.** **Mheshimiwa Spika,** jitihada za kuendeleza elimu ya msingi na maandalizi zimechukuliwa kwa kufanya uhamasishaji na uandikishaji wa wanafunzi katika ngazi za Maandalizi na Msingi Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2021 jumla ya wanafunzi 79,132 wameandikishwa wakiwemo wanafunzi wa maandalizi; 29,454, na wanafunzi 49,682 wameandikishwa kuanza darasa la kwanza. **(*Angalia kiambatisho namba 6).***

**20.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ustawi wa jamii, Afisi za Wakuu wa Mikoa zimeendelea kuwapatia wananchi 4,208 wanaoishi katika mazingira magumu msaada wa Shilingi 5,000 zinazotolewa kila mwezi kupitia Afisi za Wakuu wa Wilaya. ***(Angalia kiambatisho namba 7)***.

**21.** **Mheshimiwa Spika,** katika kudhibiti na kusuluhisha migogoro inayotokana na matumizi sahihi ya ardhi, Afisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya zimeendelea kuhakikisha migogoro yote ya ardhi inafuatiliwa na kupatiwa ufumbuzi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusika na masuala ya ardhi. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2020/2021, jumla ya migogoro 500 ya ardhi imeripotiwa katika Afisi za Mikoa na Wilaya ***(Angalia kiambatisho namba 8)***.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** katika kupambana na udhalilishaji wa watoto na unyanyasaji wa kijinsia, juhudi mbali mbali zimeendelea kuchukuliwa kupitia Afisi za Mikoa na Wilaya ili kuhakikisha matukio hayo yanapungua na hatimae yanaondoshwa kabisa. Miongoni mwa juhudi zinazochukuliwa ni pamoja na kutoa elimu kwa jamii na kufuatilia matukio yaliyoripotiwa katika ngazi mbali mbali za kisheria. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi

2020/2021, jumla ya matukio 1,151 ya udhalilishaji yameripotiwa ***(Angali kiambatisho namba 9)***.

**23.** **Mheshimiwa Spika**, baada ya utekelezaji wa jumla wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, ufuatao ni utekelezaji wa kila programu kupitia mafungu 12 ya kibajeti yaliyoanzia D01 hadi D12.

**PROGRAMU ZA MAKAO MAKUU (FUNGU D01)**

**PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ**

**PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA ORTMSMIM**

**24.** **Mheshimiwa Spika,** katika kufuata taratibu za manunuzi zilizowekwa na Serikali vikao vinne (4) vya Bodi ya Zabuni vimefanyika ambavyo vimewezesha Afisi kukamilisha ujenzi wa Mtaro wenye urefu wa mita 720 uliojengwa pembeni ya barabara ya Mwera Meli sita hadi bonde la Mto wa Mwera na mtaro wenye urefu wa mita 280 kutoka Mwera Batini hadi Bwawa Jitenge, ununuzi wa chaki kwa Skuli za Maandalizi na Msingi. Aidha, Idara imekamilisha taratibu za kupata Mkandarasi wa kufanya ukarabati wa jengo la zamani la Wizara liliopo chini ya Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe ambalo litafanyiwa ukarabati kipindi kifupi kijacho.

**25.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuweka mazingira bora ya kazi kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ilitekeleza majukumu ya usimamizi wa masuala ya kiutumishi na uendeshaji, kufanya ukaguzi wa ndani wa hesabu, kufanya manunuzi ya vitendea kazi pamoja na kutoa habari na taarifa za Wizara. Idara imeratibu shughuli za uendeshaji wa Wizara kwa kufanya malipo ya huduma za uendeshaji wa Afisi, matangazo na magazeti, matengenezo ya vyombo vya usafiri vya Wizara pamoja na kufanya malipo ya safari na stahiki kwa viongozi na watumishi. Aidha, watumishi saba (7) wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika vyuo vya ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara pamoja na kulipa posha la likizo, muda wa ziada na ubani wa kufiliwa.

26. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 4,211,700,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 940,900,000** ni mishahara, **Shilingi 2,138,100,000** matumizi mengineyo na **Shilingi 1,132,700,000** ni ruzuku ya Wakala wa Ulinzi JKU na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ. Hadi kufikia Machi 2021, Idara imeingiziwa **Shilingi 1,335,497,500** sawa na asilimia **32**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 791,613,280** sawa na asilimia **84** ni mishahara na **Shilingi 416,384,220** ni matumizi mengineyo sawa na asilimia **19** na **Shilingi 127,500,000** sawa na asilimia **11** ni ruzuku.

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA KAZI ZA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

27. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti imeratibu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mipango zikiwemo kuandaa wa bajeti na mpango kazi wa Wizara, utayarishaji wa ripoti za utekelezaji na kuziwasilisha kwenye mamlaka husika, mfano ripoti utekelezaji wa Ilani ya CCM, utekelezaji wa maagizo na ahadi za viongozi wakuu na ripoti za utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Idara imekamilisha rasimu ya awali ya Mpango Mkuu wa Utafiti ambapo maeneo 77 yamebainishwa yanahitaji kufanyiwa tafiti katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi na Idara zilizo chini ya Wizara. Aidha, Idara imeratibu upatikanaji wa majibu ya maswali yaliyoulizwa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa Wizara.

28. **Mheshimiwa Spika,** Idara imefanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Wizara na kufanya ziara za kufuatilia na kutathmini miradi ya maendeleo iliyotekelezwa kupitia fedha za mapato ya ndani yanayokusanywa na Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri Unguja na Pemba. Katika ziara hizo miradi ya Wadi iliyotekelezwa ni 16, Unguja 10 Pemba sita (6) iliyohusisha Wadi 16 kati ya wadi 110 zilizopo Zanzibar. Vile vile, Miradi ya maendeleo 11 inayoratibiwa na Tume ya Mipango Zanzibar imefuatiliwa na kutathminiwa ambapo changamoto kubwa ya kutokamilika kwa wakati miradi hiyo inatokana na kutekeleza miradi mingi kwa wakati mmoja na kuchelewesha taratibu za manunuzi. Hivyo, Wizara imejipanga

kuondosha kasoro zilizojitokeza katika kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo.

29. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 588,000,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 188,000,000** ni mishahara na **Shilingi 400,000,000** matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2021, Idara imeingiziwa **Shilingi 223,168,668** sawa na asilimia **38**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 164,672,970** sawa na asilimia **88** ni mishahara na **Shilingi 58,495,698** sawa na asilimia **15** kwa matumizi mengineyo.

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA**

30. **Mheshimiwa Spika**, kupitia programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba, Afisi kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Afisi Kuu Pemba imefanya ufuatiliaji wa kazi za kawaida, kufanya utafiti kwa lengo la kuangalia uwelewa wa wananchi juu ya Ugatuzi ambapo changamoto mbali mbali zilibainika katika nyanja ya Elimu, Afya na Kilimo. Ziara za kuangalia utekelezaji wa miradi ya Wizara kwa Pemba zilifanyika kwa mashirikiano na Tume ya Mipango Zanzibar. Aidha, katika kuratibu masuala ya utumishi na uendeshaji wa Wizara Afisi Kuu Pemba, watumishi wawili (2) wamejengewa uwezo katika ngazi ya Shahada ya Pili katika fani Sheria na Utawala wa Umma pamoja na muda mfupi katika masuala ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

31. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, program ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 730,000,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 420,000,000** ni mishahara na **Shilingi 310,000,000** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2021, program ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba imeingiziwa **Shilingi 298,933,200** sawa na asilimia **41**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 199,259,200** sawa na asilimia **47** ni mishahara na **Shilingi 99,674,000** sawa na asilimia **32** kwa matumizi mengineyo.

**PROGRAMU NDOGO YA USAJILI NA URATIBU WA JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI (NGOs)**

32. **Mheshimiwa Spika,** mchango wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali katika maendeleo ya Zanzibar kwa mwaka 2020/2021 uliathirika na ugonjwa wa Covid 19, hivyo kupelekea Jumuiya nyingi kukosa fedha za kufanya shughuli zilizokusudiwa. Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti zilizowasilishwa katika Afisi ya Mrajis wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali zimeonesha jumla ya **Shilingi 14,856,840,438** zimepatikana kwa NGOs 59 za Unguja na **Shilingi 464,302,700** kwa NGOs saba (7) za Pemba. Fedha hizo zilielekezwa kutekeleza shughuli mbali mbali za maendeleo zikiwemo utoaji wa elimu pamoja na kuendeleza Miradi ya elimu, afya, maji kilimo, na mazingira. Kwa upande wetu wa Serikali tumepunguza muda wa usajili kutoka wiki mbili (2) hadi moja (1) kulingana na kukamilika kwa taratibu na vielelezo husika kutoka kwa waombaji. Hadi kufikia Machi ya mwaka 2020/2021 jumla ya NGOs 64 zimepatiwa usajili mpya, kati ya hizo Unguja NGOs 55 na Pemba tisa (9), NGOs 98 zimepatiwa usajili wa marejeo (Unguja 57 na Pemba 41) na kuzifanya Jumuiya Zisizo za Kiserikali Zanzibar zilizosajiliwa kisheria kufika 2,428 (2,203 Unguja na 225 Pemba).

33. **Mheshimiwa Spika**, Afisi ya Mrajisi wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali imefanya ukaguzi kwa NGOs 40 (26 Unguja na 14 Pemba) kwa lengo la kubaini uhai na ufuataji wa Sheria katika ngazi za Shehia na kuangalia utekelezaji wa kazi zao pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa mujibu wa malengo yaliyowekwa katika Katiba zao. Kufuatia ukaguzi huo NGOs 300 ziligundulika kwenda kinyume na taratibu za Sheria ikiwemo kusita kufanya kazi kwa muda mrefu ambapo hatua za kuzipatia indhari ya kufutiwa usajili wao zimefanyika. Aidha Sheria ya Jumuiya namba 6 ya mwaka 1995 imeanza kufanyiwa mapitio ambapo mikutano 11 ya kukusanya maoni imefanyika katika Mikoa yote mitano (5) ya Zanzibar ambayo imewashirikisha Wadau 650 chini ya mashirikiano na Umoja wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali Zanzibar (ANGOZA).

34. **Mhehimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, programu ndogo ya Usajili na Uratibu wa Jumuiya zisizo za Kiserikali imepangiwa kutumia

jumla ya **Shilingi 240,840,000** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2021, imeingiziwa **Shilingi 49,102,071** sawa na asilimia **20**.

**WAKALA WA ULINZI JKU**

35. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa ulinzi JKU umefanikiwa kutoa huduma ya ulinzi kwa kulinda vituo 91 pamoja na kufanya doria maeneo ya utalii na uwekezaji. Wakala kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii umefanya doria katika maeneo ya Mji Mkongwe na maeneo ya fukwe za Mazizini na Mbweni na kufanikiwa kuyatawanya na kuyaondoa makundi yote yanayoleta usumbufu kwa watalii katika maeneo hayo. Wakala umefanikiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa vitendo vya uhalifu katika maeneo mbali mbali nchini kupitia huduma za ulinzi na mfumo mkuu wa mawasiliano kwa njia ya redio katika vituo vya ulinzi na imepelekea ufanisi katika utekelezaji wa zoezi hilo. Aidha, semina za ndani kwa wapiganaji zimetolewa kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kitaalam katika kuwahudumia wageni wanapokuwa katika hoteli zetu.

36. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wakala wa Ulinzi JKU uliidhinishiwa ruzuku jumla ya **Shilingi 1,132,700,000**. Hadi kufikia Machi 2021 Wakala wa Ulinzi JKU umeingiziwa ruzuku jumla ya **Shilingi 127,500,000** sawa na asilimia **11** ya makadirio ya mwaka. Aidha, Wakala wa Ulinzi JKU ulipangiwa kuchangia **Shilingi 832,800,000** katika Mfuko Mkuu wa Hazina na hadi kufikia Machi 2021 Wakala umechangia **Shilingi 240,000,000** sawa na asilimia **29**.

**PROGRAMU KUU YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

37. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imefanikisha kuandaa miongozo, mikakati na kanuni za uendeshaji wa Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Madiwani ikiwemo Muongozo wa Wajibu na Majukumu ya Madiwani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Uendeshaji wa Kamati za Maendeleo za Mikoa, muongozo wa mawasiliano baina ya Serikali za Mitaa na Taasisi nyengine na mkakati wa Usafi kwa Serikali za Mitaa. Rasimu za miongozo hiyo zipo katika hatua ya

kupata michango ya wadau kwa kupatiwa maoni yao na kuiboresha ili hatimae mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2021/2022 iweze kutumika. Idara imefanikiwa kuandaa Kanuni ya Uendeshaji na usimamizi wa Masoko pamoja na maeneo ya biashara zikiwemo Kanuni ya adhabu za papo kwa papo zinazohusu usafi na kanuni za ushuru wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Idara imekamilisha kuchapisha nakala za vitabu vya Muongozo wa upangaji Mpango Shirikishi Jamii wa fursa na vikwazo kwa maendeleo na kuvisambaza kwa wadau kwa matumizi. Aidha, kufuatia kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka (2020-2025) Idara imeratibu uundaji wa Mabaraza ya Wadi 110 na Kamati za mashauriano za shehia 388 ili kuwawezesha wananchi kushiriki katika mipango ya Mkoa.

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA SERIKALI ZA MITAA**

38. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu ya Uratibu wa Serikali za Mitaa huduma za uendeshaji wa skuli za maandalizi na msingi zimetolewa kwa kuwapatia posho wasaidizi 727 na waratibu 13 wa vituo vya TUTU, na malipo kwa Kampuni za Ulinzi za *UMAWA* na *SMART SECURITY* ambazo zinatoa huduma za ulinzi wa Skuli za msingi na maandalizi Unguja na Pemba. Idara imefanikiwa kuratibu zoezi la usafirishaji wa Madawati 3,295 (2,290 Unguja, na 1005 Pemba) katika skuli za Maandalizi na Msingi pamoja na usambazaji wa vifaa vya elimu vilivyotolewa msaada na Jumuiya ya Wakorea ijulikanayo kwa jina la "*Good Neighbour*". Aidha, Idara imeratibu zoezi la kupatiwa lishe wanafunzi katika skuli 27 za Maandalizi na Msingi (16 Unguja na 11 Pemba) ambapo mikataba kwa vikundi 78 vya wakulima wanaosambaza vyakula katika skuli mbali mbali imefungwa.

39. **Mheshimiwa Spika,** kwa kushirikiana na Shirika la kuhudumia watoto (UNICEF) Idara imefanya ujenzi wa sehemu za kuosha mikono katika skuli 22 (16 Unguja na Pemba 6) pamoja na ujenzi wa vyoo katika Skuli kumi 10 za maandalizi na msingi, (Unguja saba 7 na Pemba tatu 3). Vile vile, mikutano iliyowashirikisha Waalimu Wakuu na Wenyeviti wa Kamati za Maendeleo ya Skuli imefanyika kwa lengo la kupiga kampeni za kuwarejesha wanafunzi Skuli baada ya kufunguliwa, Skuli zilizofungwa

kufuatia mripuko wa maradhi ya Covid -19 ambapo ilionekana mahudhurio ya wanafunzi hayaridhishi.

40. **Mheshimiwa Spika,** jukumu la matengenezo ya barabara za ndani limetekelezwa kwa kufanya matengenezo ya barabara ya Masingini - Hawaii yenye urefu wa kilomita mbili (2km), ambapo jumla ya **Shilingi 668,485,000** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo na hadi kufikia Machi 2021 ujenzi umekamilika kwa hatua ya tabaka la kwanza la lami.

41. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kupitia programu Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 9,065,090,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 192,000,000** ni mishahara, **Shilingi 4,976,860,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 1,000,000,000** kwa mradi wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2021, imeingiziwa **Shilingi 1,701,677,866** sawa na asilimia **19**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 179,596,330** sawa na asilimia **94** ni mishahara, **Shilingi 1,172,081,536** sawa na asilimia **24** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 350,000,000** sawa na asilimia **35** kwa mradi wa maendeleo.

**PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI NA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SMZ**

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SMZ**

42. **Mheshimiwa Spika,** katika kuwajengea uwezo Maafisa na Wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ, Idara imewapatia mafunzo msasa Maafisa 46 wa Idara Maalum za SMZ, 38 Zimamoto na Uokozi na wanane (8) Chuo cha Mafunzo pamoja na kutoa mafunzo ya maafisa wanafunzi (Advanced) kwa Maafisa 41 (30 Chuo cha Mafunzo na 11 Zimamoto na Uokozi) yametolewa, lengo la mafunzo haya ni kuwajengea uwezo wa kiutendaji maafisa wa Zimamoto na Uokozi na Chuo cha Mafunzo Unguja na Pemba ili waweze kushiriki katika shughuli na operesheni za ulinzi na usalama ndani na nje ya Tanzania.

43. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Ulinzi na Usalama nchini, Idara imekamilisha ufungaji wa kamera katika miji ya Chakechake, Mkoani na Wete kwa Pemba. Idara inaendelea na Ufungajiwa Kamera za Ulinzi na Usalama (CCTV) awamu ya pili katika maeneo ya Kiembe Samaki –Baraza la Wawakilishi na Mazizini – Buyu, vile vile Idara inaendelea na matayarisho

ya uwekaji wa miuondo mbinu ya uwekaji wa *CCTV camera* katika maeneo ya Amani – Mboriborini na Shaurimoyo, Amani – Mwera, Mtoni – Bububu na Mombasa - Fumba.

**44.** **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza maendeleo ya viwanda nchini Kiwanda cha Ushoni cha Idara Maalum za SMZ kilichopo KVZ Mtoni, kimefanikwa kuzalisha jumla ya jozi 1,280 ya sare za wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ na jozi 410 kwa Wakala wa Ulinzi JKU zenye thamani ya **Shilingi 51,520,000**. Kiwanda kimefanikiwa kushona nguo za Makampuni mbali mbali zenye thamani ya **Shilingi 31,068,163**. Aidha, kiwanda kinaendelea kufanya tathmini ya uwezo wa mahitaji kwa lengo la kutambua mahitaji halisi ya uzalishaji wa Kiwanda cha Ushoni wa nguo na viatu ili kukidhi mahitaji ya Idara Maalum pamoja na wananchi wa Zanzibar.

**45.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Programu ndogo ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 13,460,000,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,960,000,000** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 10,500,000,000** kwa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2021, imeingiziwa **Shilingi 9,672,838,083** sawa na asilimia **71**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,036,246,605** sawa na asilimia **35** kwa matumizi ya kawaida na **Shilingi 8,592,580,478** sawa na asilimia **82** kwa miradi ya maendeleo.

## PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA UTUMISHI WA IDARA MAALUM ZA SMZ

**46.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Utumishi wa Idara Maalum za SMZ, Tume ya Utumishi wa Idara Maalum za SMZ imefanya vikao viwili (2) vya kawaida ambavyo vimejadili na kupandisha vyeo maafisa wadogo 123 (KZU 43, Mafunzo 42 na JKU 38) na kupendekeza kwa mamlaka husika kupandishwa vyeo kwa maafisa waandamizi 60 (Mafunzo 28, KMKM 17 na KZU 15). Aidha Tume imepokea jumla ya malalamiko 90 kutoka kwa waliokuwa watumishi wa Idara Maalum za SMZ ambao wamelalamika kutolipwa stahiki zao zikiwemo kiinua mgongo, pencheni pamoja na kuachishwa na kufukuzwa kazi kinyume na taratibu za kisheria, ambapo malalamiko yote yalijadiliwa na kutolewa maamuzi. Tume ilifanya vikao

viwili (2) na wadau wa Sheria kujadili rasimu ya pili ya Sheria No. 6 ya mwaka 2007 ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ ambayo ipo katika hatua ya kufanyiwa marekebisho.

**47.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ iliidhinishiwa ruzuku ya **Shilingi 156,000,000**. Hadi Machi 2021, Tume iliingiziwa **Shilingi 44,011,000** sawa na asilimia **28**.

## PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU D02-D06)

**48.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Idara Maalum za SMZ zimetekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu 10 ambapo kila Fungu limetekeleza programu kuu mbili. Maelezo yafuatayo yanahusu utekelezaji wa programu hizo kuanzia Fungu D02 hadi D06.

## JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) - FUNGU D02

**49.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu ya Mafunzo kwa vijana, Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar (JKU) limeendelea kutoa mafunzo ya uzalendo na uzalishaji mali kwa vijana 5,582. Kati yao, Vijana 3,000 wanaendelea na mafunzo ya uzalendo na uzalishaji mali katika Kambi za JKU Unguja na Pemba, vijana 1,238 wanaendelea na mafunzo ya amali katika fani za useremala, umeme, ufundi uwashi, ushoni, ufundi bomba, ufundi magari, na ufundi mchundo katika Skuli ya Ufundi ya JKU Mtoni na wanafunzi 1,344 wanaendelea na masomo katika mchipuo wa biashara, sayansi na kompyuta katika skuli ya JKU Sekondari Mtoni. Aidha, vijana 1,714 wamemaliza mafunzo yao ya uzalendo mnamo mwezi Disemba, 2020 ambao wameruhusiwa kutoka kambini kwenda kutumia mafunzo waliyoyapata katika kujitafutia maisha.

**50.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia shughuli za uzalishaji mali, Jeshi la Kujenga Uchumi limefanikiwa kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa kilimo cha umwagiliaji wa ekari 72 katika bonde la Msaani na Kwapweza pamoja na kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa ufugaji wa Kisasa wa Samaki katika Kambi ya JKU Mwambe kisiwani Pemba. Ripoti za upembuzi yakinifu zimeonesha umuhimu wa kufanya miradi hiyokatika maeneo

yaliyopendekezwa ili kuongeza uzalishaji na usalama wa upatikanaji wa chakula. Aidha, Wapiganaji 60 wanaendelea na mafunzo ya ugani yanayoendeshwa na wataalamu wa ndani ya Kikosi kwa lengo la kuwa na wakufunzi wazuri wa kuwafundisha vijana wanaojiunga JKU na kupata stadi za uzalishaji wa mazao ya kilimo. JKU imeshiriki vyema katika maonesho ya siku ya wakulima (Nane nane) yaliyofanyika Dole na siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika Chamanangwe mwaka 2020 na kupewa tunzo ya ushindi wa kwanza katika maonesho hayo.

**51.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mifugo JKU inafuga kuku wapatao 16,000 wakiwemo 4,000 wa nyama na 12,000 mayai, JKU ina boti nne za uvuvi ambazo zinaendelea kuvua samaki kwa wastani wa tani 1.3 kwa mwezi. Aidha katika kuendeleza Mpango wa Kitaifa wa kilimo cha mpunga nchini, wastani wa ekari 202 za mpunga wa kutegemea mvua zimelimwa Unguja na Pemba na ekari 10 za mpunga wa umwagiliaji maji katika Bonde la JKU Cheju. Kambi za kilimo na ufugaji zimepatiwa pembejeo ikiwemo mbolea na mbegu za mboga mboga, ambapo ekari 20 zimelimwa za papai, tungule, matikiti, vitunguu maji na aina mbali mbali za mboga mboga. Aidha, samani za ofisi na nyumbani zimezalishwa kupitia kiwanda cha uchongaji kilichopo Saateni.

**52.** **Mheshimiwa Spika,** katika Programu ya Utawala na uendeshaji, jumla ya Askari 250 wameshiriki mafunzo ya uongozi mdogo wa kijeshi. Maafisa na wapiganaji 100 walipatiwa posho za likizo, watumishi 14 walijengewa uwezo katika fani za Afya, Elimu, Uchumi, Uhasibu na Kilimo kati ya hao13 katika ngazi ya shahada ya kwanza na mmoja katika ngazi shahada ya uzamivu (PhD). Aidha, huduma ya chakula, usafiri, vifaa vya kuandikia, mawasiliano, mazishi, fidia, vifaa vya ofisini na matengenezo ya vifaa vya usafiri zimetolewa pamoja na huduma za Afya ya kinywa na meno, mama na mtoto, vipimo vya malaria na ini zimetolewa kwa Maafisa, Wapiganaji na wananchi. Timu za mpira za JKU wanaume na wanawake zimeendelea kushiriki ligi na mashindano mbali mbali ikiwemo ligi kuu ya Zanzibar.

**53.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi ya maendeleo, Jeshi la Kujenga Uchumi linatekeleza miradi ya maendeleo ya ujenzi wa Skuli ya Ufundi ya JKU Mtoni na Mradi wa Mahanga na nyumba za Askari Msaani Pemba.

Mradi wa Skuli ya Ufundi JKU Mtoni upo katika hatua ya usimamishaji wa nguzo ya ghorofa ya pili na kufunga bimu za ghorofa ya pili ili hatimaye kuezeka na mradi wa Mahanga na nyumba za Askari Msaani Pemba ujenzi wake umefikia hatua ya umaliziaji wa uwekaji wa mfumo wa umeme na upigaji wa plasta kwa majengo yote matatu ili kuweka milango na madirisha pamoja na uwekaji wa sakafu.

54. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Jeshi la Kujenga Uchumi lilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 31,557,600,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 24,066,000,000** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 2,991,600,000** matumizi mengineyo na **Shilingi 4,500,000,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2021, Jeshi la Kujenga Uchumi limeingiziwa jumla ya **Shilingi 22,564,450,580** sawa na asilimia **72**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 20,215,616,920** sawa na asilimia **84** ni mishahara, **Shilingi 1,392,506,000** sawa na asilimia **47** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 956,327,660** sawa na asilimia **21** kwa kazi za maendeleo. Aidha, Jeshi la Kujenga Uchumi limepangiwa kuchangia **Shilingi 87,224,000** katika Mfuko Mkuu wa Hazina na kuchangia **Shilingi 18,932,000** sawa na asilimia **22**.

**CHUO CHA MAFUNZO (MF) – FUNGU D03**

55. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ya urekebishaji tabia Kikosi kimepokea jumla ya wanafunzi na mahabusu 2,469, kati yao wanafunzi ni 637 na mahabusu 1,832. Aidha, wanafunzi 205 waliruhusiwa kutoka na wanafunzi 68 walipata msamaha wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. Kikosi kimeendelea kutoa elimu ya watu wazima kwa wanafunzi na mahabusu wasiojua kusoma na kuandika ambapo jumla ya wanafunzi 20 wamefanikiwa kufanya mitihani kwa ushirikiano na Idara ya Elimu Mbadala ambapo wanafunzi 76 wanaendelea na kisomo cha watu wazima kwa Kambi ya Kiinua Miguu Unguja na Kangagani Pemba. Juhudi za kuhamasisha wanafunzi pamoja na kutanua mafunzo ya kujua kusoma na kuandika kwa Kambi nyengine za Unguja na Pemba zinaendelea. Chuo cha mafunzo kimeendelea kuwapatia wanafunzi wake mafunzo katika fani za ushoni, kilimo, ufundi ujenzi, ufundi chuma, ufundi seremala, ufundi gari, ufugaji na utunzaji wa bustani.

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa shughuli za Uzalishaji Idara imevuna zao la miwa eka 75 sawa na tani 270 zilizouzwa kiwanda cha sukari Mahonda, maeneo mengine ya uzalishaji yanayohusisha kilimo cha muhogo, mahindi, mpunga pamoja na viazi yanaendelea kuimarishwa ili kupata chakula kuwalisha wanafunzi, mahabusu na maaskari wanaokuwa zamu. Kikosi kimezipatia Kambi zake Pembejeo za kilimo pamoja na kuendelea na utengenezaji wa miundo mbinu ya kilimo cha umwagiliaji katika kambi ya Langoni. Aidha, Kikosi kimeshapata mshauri elekezi wa kufanya upembuzi yakinifu kwa mradi wa umwagiliaji katika Kambi ya Kinumoshi ambapo kazi hiyo itafanyika rasmi mwezi wa Juni 2021.

57. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa programu ya Utawala na Uendeshaji, Chuo cha Mafunzo kimeendelea kutoa huduma za kiutawala kwa kuwapatia chakula wapiganaji na wanafunzi, ununuzi wa vifaa vya ofisi, mafuta pamoja na kufanya matengenezo ya kawaida ya magari. Kikosi pia kimefanya ununuzi wa dawa kwa kambi zote za Unguja na Pemba na kuwapatia mafunzo maafisa na wapiganaji watano (5) katika fani za

uhasibu, umeme, uchumi, rasilimali watu pamoja na fani ya uhusiano wa kimataifa. Aidha, Kikosi kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wapiganaji 18 katika fani ya urekebishaji sambamba na kuwapatia mafunzo ya uaskari wapiganaji 276 kwa kambi za Unguja na Pemba. Kwa upande wa michezo timu ya mpira wa miguu na mpira wa mikono zimeshiriki mashindano ya ligi kuu ya Zanzibar. Kikosi pia kimeimarisha vikundi vya sanaa na taarabu kwa lengo la kuelimisha pamoja na kutoa burudani.

**58.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kazi za maendeleo, Chuo cha Mafunzo kimekamilisha ujenzi wa jengo la urekebishaji tabia wanafunzi watoto katika kambi ya Hanyegwa Mchana, hatua inayoendelea ni uwekaji wa vifaa kwa ajili ya kuanza huduma. Kwa upande wa Kambi ya Wete Pemba ujenzi wa jengo la Afisi Kuu ya Zoni upo katika hatua ya uwekaji jamvi kwa ajili ya kuanza na ghorofa ya kwanza. Aidha, taratibu za kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Chuo Cha Mafunzo cha kisasa Hanyegwa Mchana zinaendelea.

**59.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Chuo cha Mafunzo kiliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 21,865,600,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 17,276,200,000** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 3,089,400,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 1,500,000,000** kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2021, Chuo Cha Mafunzo kimeingiziwa **Shilingi 14,263,457,810** sawa na asilimia **65**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 12,569,154,610** ni mishahara sawa na asilimia **73**, **Shilingi 1,444,303,200** matumizi mengineyo sawa na asilimia **47** na **Shilingi 250,000,000** sawa na asilimia **19** kwa ajili ya kazi za maendeleo. Aidha, Kikosi kiliidhinishiwa makusanyo ya mapato ya Hazina ya **Shilingi 75,720,000** na kukusanya **Shillingi 42,074,000** sawa na asilimia **56**.

**KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)- FUNGU D04**

60. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ya Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimeimarisha ulinzi wa doria, uokozi na udhibiti wa magendo katika ukanda wote wa bahari na nchi kavu ya Visiwa vya Unguja na Pemba kwa lengo la kudhibiti hali ya usalama, magendo na uchafuzi wa mazingira baharini. Matukio mbali mbali ya utoroshaji wa bidhaa yaliweza kudhibitiwa kwa kukamata bidhaa mbalimbali ambazo zimekabidhiwa kwa mamlaka husika ambapo jumla ya matukio 28 yaliripotiwa na kuchukuliwa hatua za kisheria. Katika shughuli zake hizo pia Kikosi kimeweza kuokoa jumla ya waathirika 30 waliopata majanga ya kuzama na kuharibikiwa na vyombo baharini.

61. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha shughuli za uzamiaji na uokozi, Kikosi kimeendelea kununua vipuri mbali mbali kwa ajili ya Boti zake kubwa na ndogo pamoja na kuzifanyia matengezo gari zinazotowa huduma na kufanya ukarabati wa vituo vya ufundi. Kikosi kimeendelea kununua mafuta kwa ajili ya shughuli mbali mbali za doria na ulinzi wa nchi kavu na baharini. Aidha, Kikosi kimenunua gari tano mpya kwa ajili ya shughuli za operesheni mbali mbali.

62. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Huduma za KMKM, Kikosi kimeweka mazingira mazuri ya kazi na ustawi wa wapiganaji kwa kutoa huduma ya chakula kwa Maafisa na wapiganaji wake Unguja na Pemba, kufanya ununuzi wa vitanda na magodoro kwa makambi, ununuzi wa sare kwa maafisa na wapiganaji pamoja na sare maalum kwa ajili ya sherehe za miaka 56 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Kikosi kimewapatia stahiki Maafisa na wapiganaji pamoja na kufanya safari za Kikazi za ndani kwa lengo la kuimarisha ufanisi na utendaji. Aidha, huduma za afya zimetolewa katika vituo vyake vya afya pamoja na kuwapatia matibabu maafisa wapiganaji na wananchi ambapo jumla ya watu 83,770 wamepatiwa huduma ya afya katika hospitali ya KMKM Kibweni.

63. **Mheshimiwa Spika,** Kikosi kimewajengea uwezo maafisa na wapiganaji wake kwa kutoa semina endelevu katika kada mbali mbali za kiutendaji na utoaji huduma, kuwaendeleza kitaaluma watendaji wake 44, wanaosoma vyuo mbali mbali vilivyomo ndani na nje ya nchi kwa kada tofauti ambazo ni afya, Ubaharia, Utawala na ufundi kwa viwango tofauti ambao, ni Shahada ya Uzamili watatu (3), Shahada ya kwanza wanane (4), Stashahada na Cheti 28. Sambamba na hilo, kikosi kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wapiganaji wake ikiwemo, mawasiliano, uokozi na uzamiaji, afya, utunzaji nyaraka na kumbukumbu za Ofisi Unguja na Pemba pamoja na mafunzo juu ya sheria mpya ya magendo kwa wapiganaji wetu.

64. **Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha makaazi ya wapiganaji, Kikosi kimeendelea kufanya matengenezo ya Majengo ya Kambi za Kibweni, Kibwengo na Kama kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba kambi za Wete na Sengenya. Aidha Kikosi kimejenga kambi mpya ya Kiuyu-Micheweni Pemba pamoja na kumalizia upembuzi yakinifu wa Ujenzi wa Kituo cha mafunzo ya Uzamiaji na Uokozi na Ujenzi wa gati ndogo ambao umeshakamilika na ripoti zake kuwasilishwa Tume ya Mipango Zanzibar.

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimeidhinishiwa **Shilingi 35,630,700,000**. Kati ya hizo **Shilingi 5,586,800,000** kwa matumizi mengineyo, **Shilingi 24,543,800,000** kwa matumizi ya mishahara na maposho na **Shilingi 5,500,000,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2021, Kikosi kimeingiziwa **Shilingi 23,414,549,866** sawa na asilimia **66**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 18,503,404,700** sawa na asilimia **75** kwa mishahara na maposho, **Shilingi 2,928,241,206** sawa **52** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 1,982,893,960** sawa na asilimia **36** kwa miradi ya maendeleo. Aidha, Kikosi kiliidhinishiwa makusanyo ya **Shilingi 60,542,000** kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina na kukusanya **Shilingi 25,000,000** sawa na asilimia **41**.

## KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) - FUNGU D05

66. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kilipanga kutekeleza programu kuu mbili ambazo ni

Programu ya Uzimaji Moto na Uokozi na Programu ya Utawala na Uendeshaji. Kupitia programu ya uzimaji moto na uokozi Kikosi kimefanikiwa kuyafikia matukio 158 ya moto yaliyoripotiwa kwa kipindi cha Julai – Machi, 2020/2021 ambapo Kikosi kilifanikiwa kuwakoa watu 25 wakiwa hai na watu 9 wakiwa wamefariki pamoja na kuokoa kiasi cha **Shilingi 1,839,000,000** kwa makisio. ***Angalia Kiambatisho namba 10***. Hali hii inaonesha kupungua matukio ya moto nchini kwa asilimia 27, ikilinganishwa na matukio 216 yaliyoripotiwa mwaka 2019/20 na matukio 265 kwa mwaka 2018/19. Kupungua huko kumetokana na mpango wa kuelimisha jamii na taasisi za umma na binafsi kupitia vipindi 23 vya televisheni na 11 vya redio 23 vilivyotayarishwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC), pamoja na taasisi 33 za Serikali na 44 binafsi zilizoelimishwa juu ya namna ya hadhari za moto na hatua za kuchukua unapotokezea.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** hadhi ya uwanja wetu wa ndege na bandari kitaifa na kimataifa imedumishwa kwa kuhakikisha huduma za zimamoto na uokozi zinapatikana muda wote. Kikosi kimehudumia safari za ndege ndogo 3,787 na ndege kubwa 768 wakati wa kutua, kuruka na kutia mafuta pamoja na kuhudumia safari 564 za Boti za abiria meli 134 za abiria na mizigo katika Bandari. Aidha, Boti ya Zimamoto imefanya doria za mara kwa mara kwa lengo la kuimarisha usalama wa vyombo vya baharini pamoja na maisha ya wananchi na mali zao. Aidha, Kikosi kimefungua kituo kipya cha Zimamoto Kijichame Wilaya ya Micheweni na kufanya matengenezo makubwa ya vituo vya zimamoto na uokozi Chanjaani, Kigunda, Kwerekwe na Marumbi ili kuimarisha huduma za zimamoto mijini na vijijini.

**68.** **Mheshimiwa Spika,** kupitiaprogramu ya utawala na uendeshaji Kikosi kimewajengea uwezo wapiganaji 291 na maafisa 66 kwa kuwapatia mafunzo ya kiutendaji na kitaaluma ili kukuza utendaji wao wa majukumu. Stahiki kwa wapiganaji 156 na maafisa 22 zimelipwa ambazo zimehusisha posho za likizo, uhamisho na safari za kikazi. Vilevile, malipo ya ununuzi wa vifaa vya uokozi na uzimaji moto, vifaa vya kiaskari, vifaa vya ofisini na chakula cha maafisa na wapiganaji wanaokuwa zamu yamefanyika.

69. **Mheshimiwa Spika**, Kikosi kimeunga mkono na kutekeleza kivitendo agizo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Dkt Hussein Ali Mwinyi la uwekaji wa miji safi kwa kujenga njia ya watembea kwa miguu mita 258 katika eneo la Kilimani pembezoni ya barabara ya Mnazi Mmoja hadi Kiembesamaki Uwanja wa Ndege. Kwa upande wa michezo, timu ya mpira wa miguu imeendelea kushiriki ligi kuu ya Zanzibar, Kombe la ligi (FA), na Timu ya mpira wa pete imeshiriki mashindano ya ligi kanda ya Unguja, Kombe la Muungano na kombe la Afrika Mashariki.

70. **Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika kutekeleza mradi wa maendeleo wa ujenzi wa mahanga na vituo vya Uzimaji moto na Uokozi, ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokozi Kijichame umefikia asilimia 80 ambapo kwasasa matukio ya ajali katika Wilaya ya Micheweni yanahudumiwa na kituo hicho imetokana na kukamilika kwa sehemu ya chini ya jengo pamoja na upatikanaji wa gari. Aidha, taratibu za kumpata mzabuni wa ununuzi wa gari mbili za kisasa za zimamoto zimekamilika hatua inayofuata ni mzabuni huyo kufanyiwa malipo na Tume ya Mipango Zanzibar.

71. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kikosi kiliidhinishiwa **Shilingi 16,795,900,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 11,652,000,000** kwa ajili ya mishahara na maposho, **Shilingi 2,643,900,000** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 2,500,000,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2021, Kikosi kimeingiziwa **Shilingi 10,188,321,321** sawa na asilimia **61**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 8,848,543,821** sawa na asilimia **76** kwa ajili ya mishahara na maposho, **Shilingi 1,139,777,500** sawa na asilimia **43** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 200,000,000** sawa na asilimia **8** kwa kazi za maendeleo. Kwa upande wa mapato, Kikosi kiliidhinishiwa kukusanya mapato ya **Shilingi 45,700,000** na kufanikiwa kukusanya **Shilingi 22,670,000** sawa na asilimia **50** ya makadirio ya mwaka.

**KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ) - FUNGU D06**

72. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kikosi cha Valantia kilipangiwa kutekeleza Programu Kuu mbili ambazo ni Programu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali Zao na Programu ya Utawala na Uendeshaji.

KupitiaProgramu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao Kikosi kimefanya doria katika maeneo mbali mbali; kimefikisha wapiganaji katika vituo vya ulinzi kwa wakati pamoja na kutoa huduma za chakula kwa wapiganaji waliokuwa katika shughuli za ulinzi. Wapiganaji 699 wamepatiwa mafunzo maalum ya askari wa miguu; Wapiganaji 120 wamepatiwa mafunzo ya Ukufunzi yaliyoendeshwa na wakafunzi wa Jeshi la Wananchi Tanzania na wapiganaji 62 wamepatiwa mafunzo maalum ya kuzuia ghasia kwa haraka. Aidha, huduma za afya zimekuzwa kwa kutanua wigo wa utoaji wa matibabu kwa wapiganaji Unguja na Pemba pamoja na kuwapatia maafisa na wapiganaji elimu juu ya athari za ugonjwa wa homa ya ini na athari ya mripuko wa ugonjwa wa homa ya mafua makali yajulikanyao kwa jina la Corona (Covid-19).

**73.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ya utawala na uendeshaji Kikosi kimenunua vifaa vya Ofisini; kuwapatia likizo na Stahiki zao baadhi ya Maafisa na wapiganaji; na kufanya matengenezo ya vyombo vya usafiri na matengenezo ya majengo madogo ya kambi. Timu ya Mpira wa Miguu wanaume ilifanikiwa kuchukua ubingwa wa Kombe la ZFA, hivyo kuiwakilisha Zanzibar katika Kombe la shirikisho Barani Afrika. Kwa upande wa Timu ya mpira wa Kikapu ya Wanawake KVZ imefanikiwa kuchukua ubingwa wa kanda ya Zanzibar. Aidha kwa upande wa sanaa na utamaduni Kikosi kimepata medani kwa mchezo wake uliopewa jina la Uchaguzi wa Amani katika mashindano yaliyofanyika katika Hoteli ya Madina-tul-Bahar iliyopo Mbweni Zanzibar.

**74.** **MheshimiwaSpika,** kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kikosi kinaendelea na mradi ujenzi wa Ofisi, Nyumba, Hanga na Kibanda cha Ulinzi katika Kambi ya Pujini – Pemba ambapo kwa sasa Hanga moja limekamilika kwa kufikia hatua ya uezekaji wa paa. Kikosi kimekarabati Ofisi ya Mkuu wa Kikosi Makao Makuu Mtoni; ukuta ulioanguka katika Kambi ya Mtoni pamoja na hanga linalotumika kama darasa katika Chuo cha KVZ – Pangatupu. Kadhalika, Kikosi kimeandaa andiko la mradi wa Ufugaji wa Samaki katika Kambi ya KVZ Mto wa Maji baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu, hatua iliyofikia kwa sasa ni kupata maoni ya

wadau na hatimae andiko hilo kuwasilishwa Tume ya Mipango kwa hatua zaidi.

**75.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kikosi cha Valantia kiliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 15,727,625,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 12,047,625,000** ni mishahara, **Shilingi 2,180,000,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 1,500,000,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2021 Kikosi kiliingiziwa **Shilingi 13,519,102,789** sawa na asilimia **86**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 11,776,063,789** sawa na asilimia **98** ni mishahara, **Shilingi 1,443,039,000** sawa na asilimia **66** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 300,000,000** sawa na asilimia **20** kwa kazi za maendeleo.

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (FUNGU D07-D11)**

**76.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mikoa imetekeleza Programu Kuu tatu ambazo ni Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Serikali katika Mkoa, Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Mkoa, Wilaya na Shehia, na Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Naomba kutumia nafasi hii kutoa ufafanuzi wa utekelezaji wa programu za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kila fungu;

**MKOA WA MJINI MAGHARIBI - FUNGU (D07)**

**77.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mkoa wa Mjini Magharibi kupitia programu zake tatu ulipanga kuimarisha hali ya usalama katika Mkoa; kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto; kuendeleza dhana ya utalii kwa wote, kutatua migogoro inayojitokeza ndani ya jamii; kusimamia na kutoa ushauri kwa shughuli zinazotekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mkoa pia ulipanga kuandaa nyaraka za miradi midogo midogo kwa lengo la kuwasaidia vijana kujiajiri katika sekta ya utalii na kilimo.

**PROGRAMU YA KUSIMAMIA SHUGHULI ZA SERIKALI KATIKA MKOA**

**78.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha hali ya usalama ndani ya Mkoa, jumla ya vikao 36 vya kawaida na 10 vya dharura vya Kamati za Usalama za

Mkoa vimefanyika ambavyo vilijadili ufanikishaji wa Sherehe na matukio ya Kitaifa yaliyojitokeza, hali ya vitendo vya udhalilishaji na matukio mbalimbali ya uvunjifu wa amani, mikakati ya kuviimarisha vikundi vya polisi jamii na utekelezaji wa maagizo ya Viongozi wa Kitaifa. Mikutano mitatu (3) imefanywa kwa lengo la kusikiliza kero za kiusalama ndani ya Shehia na kuzitafutia ufumbuzi ambapo mafunzo maalum yametolewa kwa vikundi saba (7) vya polisi jamii vilivyoundwa upya. Aidha, ziara na doria 28 zilifanywa katika maeneo yenye changamoto za kiusalama na kufanikiwa kukamata gari nne za n'gombe zilizotumiwa katika shughuli za uchimbaji wa mchanga kinyume na sheria pamoja na kukamatwa watu 36 waliotuhumiwa kujihusisha na vitendo vya uhalifu wamefikishwa katika vyombo vya Sheria.

79. **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Udhalilishaji, Mkoa umefanikisha kukamatwa kwa watuhumiwa watano (5) wa vitendo vya udhalilishaji na kufuatilia matukio 648 yaliyoripotiwa katika ngazi za Wilaya. Kati ya matukio hayo, matukio 47 yapo Mahakamani, 155 yanaendelea na upelelezi katika vituo vya Polisi, 19 yapo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka; moja (1) limetolewa hukumu na moja (1) limefutwa. Aidha, matukio 172 ya utelekezaji wa watoto yamepatiwa ufumbuzi na matukio 253 yanaendelea na hatua za ufumbuzi. Aidha, mafunzo maalum ya Malezi ya watoto yametolewa kwa walezi 45 wanaotarajiwa kulea watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwa lengo la kuhakikisha wanatoa huduma nzuri kwa watoto watakaokabidhiwa.

80. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza maagizo yanayotolewa na Viongozi wa Kitaifa wakati wa ziara zao katika maeneo mbalimbali, Mkoa, uliagizwa kuwatafutia wafanyabiashara wadogo wadogo wa Kijangwani, Darajani na maeneo yasiyo rasmi eneo maalum la kufanyia shughuli zao bila ya kubugudhiwa na kusumbuliwa. Kwa mnasaba huo, Mkoa umefanikisha ujenzi wa soko la muda la Kibandamaiti ambalo limefunguliwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi na kupelekea wafanyabiashara wadogo zaidi ya 1,500 kunufaika. Kwa upande wa agizo la kuimarisha usafi wa mji. Mkoa umesimamia utekelezaji wa agizo la kuifanya barabara inayotoka Uwanja

wa Ndege hadi Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya mfano katika usafi. Barabara hiyo kwa sasa muonekano wake unavutia kufuatia kujengwa michirizi, njia za waendao kwa miguu, upandaji wa miti na bustani pamoja kupakwa rangi majengo yaliyopo katika barabara hiyo.

81. **Mheshimiwa Spika,** Mkoa umeratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Kisekta ambapo kwa upande wa Sekta ya Elimu, Mkoa umetembelea skuli 46 ikiwemo (28 Sekondari na 18 msingi) kwa lengo la kusikiliza na kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya elimu. Kufuatia changamoto hizo vikao viwili vimefanyika vilivyowashirikisha wadau wa maendeleo ya elimu na Walimu Wakuu wa Skuli za Msingi na Sekondari ndani ya Mkoa. Miongoni mwa mikakati iliyokubaliwa katika vikao hivyo ni kuwataka Walimu Wakuu na Walimu wa Taaluma kuwasimamia Walimu katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya mitihani ya Taifa ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi na kutokomeza divisheni zero katika Mkoa. Aidha, Mkoa kwa mashirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali umeratibu utatuzi wa changamoto ya upungufu na walimu wa Sayansi hususan kwa somo la Fizikia.

82. **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuimarisha Ustawi wa Jamii, Mkoa umetoa msaada wa magodoro 30 katika kituo cha kulelea watoto yatima cha Mazizini. Ziara Saba (7) zimefanyika kufuatilia malalamiko ya familia zenye watoto wenye ulemavu na kubaini changamoto mbalimbali zinazowakabili zikiwemo za kukosa visaidizi, mahitaji ya kujikimu na mitaji ya kuendeleza biashara zao. Katika kuzitatua changamoto hizo watu wenye ulemavu tisa (9) wamepatiwa msaada wa chakula, 18 wamepatiwa viti vya magurudumu mawili na fimbo nyeupe na 11 wamepatiwa mikopo kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao. Aidha, wananchi 411 walipatiwa msaada wa chakula na nguo kukidhi mahitaji yao ya lazima. Mkoa umeendelea kuratibu zoezi la kila mwezi la malipo ya pencheni Jamii kwa wazee waliofikia umri wa miaka 70 ambapo jumla ya wazee 8,514 wamelipwa na pia wananchi 884 wanaoishi katika mazingira magumu wamelipwa na Mkoa Shilingi 5,000 kwa mwezi.

83. **Mheshimiwa Spika,** Mkoa umefanya ufuatiliaji wa matukio mbalimbali ya maafa yaliyotokea yakiwemo matukio ya moto ambapo nyumba 31

ziliungua, nyumba 179 zimeathiriwa kwa upepo na nyumba mbili (2) zimeporomoka ambapo Mkoa umewafariji waathirika wa maafa hayo na kuwapatia misaada ikiwemo vyakula na baadhi ya vifaa vya matumizi ya nyumbani. Aidha, kufuatia taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini, elimu ya tahadhari ya mvua za Vuli na masika imetolewa kwa wananchi kupitia mikutano 23 iliyofanywa kwenye Shehia zilizomo kwenye hatari ya kupata maafa ya mvua. Vile vile, vikao sita (6) vya Kamati za Kukabiliana na Maafa za Wilaya vimefanyika kujadili hali ya maafa katika maeneo mbalimbali na kupanga mikakati ya kukabiliana na maafa.

**84.** **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana, Mkoa umesaidia upatikanaji wa eneo lenye ekari 4.5 kwa ajili ya vijana 40 kutoka Shehia tano za Magharibi "A" wanaojishughulisha na kilimo cha Tangawizi kupitia ufadhili wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) pamoja na vijana 15 wa ushirika wa uchongaji kutoka Shehia ya Chuini wamepatiwa eneo. Mkoa umeratibu usajili wa vyama vipya vya Ushirika 54 vyenye wanachama 570 na mafunzo ya stadi za maisha, habari, ujasiriamali na ufundi kwa vijana 61 chini ya msaada wa UNDP. Vile vile, kwa kushirikiana na Mashirika ya Kimaitaifa (ILO, FAO na USAID), Mkoa umefanya ziara nne (4) kwa vikundi vya vijana kuangalia fursa zilizopo na kuahidi kusaidia miradi iliyoanzishwa na inayotarajiwa kuanzishwa na vijana hao.

**85.** **Mheshimiwa Spika,** suala la utalii kwa wote limeendelea kuimarishwa ambapo Kamati tatu za Utalii zimeundwa kwa lengo la kushajihisha na kukuza utalii wa ndani. Vile vile, Mkoa umetembelea baadhi ya maeneo yenye vivutio vya utalii yakiwemo Kisiwa cha Kwale na Pango la Dimani sambamba na kuibua maeneo mapya ya utalii yakiwemo Pango la Nyamanzi na Pango la Fumba. Aidha, Mkoa umekutana na watembeza watalii wa maeneo ya visiwakwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa wageni. Sambamba na kushirikiana na Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe kuhakikisha mji huo unabakia katika asili yake ili uweze kuvutia Watalii zaidi na kuongeza ajira na mapato yatokanayo na utalii.

**PROGRAMU YA UTAWALA NA UENDESHAJI.**

86. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mahusiano na mashirikiano kati ya Mkoa na Wadau wengine, Mkoa umefanya mikutano na wadau mbalimbali wakiwemo Mabalozi wadogo waliopo Zanzibar, Wawekezaji, Wafanyabiashara, Makampuni ya Ujenzi na Taasisi za fedha. Kufuatia mikutano hiyo, Wadau wameahidi kusaidia utekelezaji wa shughuli za maendeleo na kuimarisha mahusiano ndani ya Mkoa. Kampuni za CRJE, RANS, ESTEEM na HAINAN zimejitokeza kusaidia utekelezaji wa agizo la kuimarisha usafi katika barabara ya Uwanja wa ndege – Mnazi mmoja, ambapo kampuni hizo zimegharamia pamoja na kujenga njia za waendao kwa miguu.

87. **Mheshimiwa Spika,** katika kuzipatia ufumbuzi kero za wananchi, Mkoa umeunda Madawati maalum ya kusikiliza malalamiko ambapo jumla ya migogoro 152 ya ardhi imepokelewa ikiwa ni ongezeko la migogoro 92 kutoka 60 iliyoripotiwa ya mwaka 2019/2020. Ongezeko hilo limetokana na muamko wa wananchi wa kuripoti malalamiko yao katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Mkoa. Kati ya migogoro hiyo 64 imepatiwa ufumbuzi, sita (6) ipo Mahakamani na 82 inaendelea kupatiwa ufumbuzi kwa kushirikiana na Taasisi husika. Maombi 410 yamepokelewa yaliyohusisha kupatiwa misaada ya kujikimu kimaisha na kutafutiwa ajira ambapo maombi 173 yametatuliwa. Aidha, jumla ya mikutano 29 ya Shehia imefanywa kwa lengo la kusikiliza changamoto zilizopo na kusaidia kuzipatia ufumbuzi.

88. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Programu ya Utawala na Uendeshaji, watumishi wanane (8) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani za Uchumi, Takwimu, Habari na Mawasiliano, Rasilimali Watu na Fedha na watumishi 11 wamepatiwa mafunzo elekezi ya Utumishi wa Umma katika Chuo cha Utumishi wa Umma Zanzibar. Aidha, Mkoa ulisimamia uajiri wa watumishi 125 wa kada za Uwalimu, Afya, Uchumi, Tehama, Biashara, Ulinzi na Ukatibu Muhutasi na kusimamia uhamisho wa wafanyakazi 13 ndani na nje ya Mkoa. Mkoa umezipatia Ofisi vifaa na vitendea kazi vikiwemo gari moja (1) na vifaa vya kuandikia na kulipa stahiki za wafanyakazi. Vikao 32 vyenye lengo la kuimarisha utendaji wa watumishi ndani ya Ofisi ya Mkoa, Wilaya na Mabaraza ya Manispaa vimefanywa kuhimiza uwajibikaji na nidhamu katika maeneo ya kazi.

**PROGRAMU YA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA SERIKALI ZA MITAA JIJI LA ZANZIBAR**

**89.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Jiji la Zanzibar limepanga kuanzisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Zanzibar; Kuipatia Ofisi vitendea kazi; kutoa miongozo na ushauri kwa Manispaa za Wilaya; na Kubuni na kuanzisha miradi ya kuendeleza Jiji la Zanzibar.

**90.** **Mheshimiwa Spika,** Jiji la Zanzibar limeweza kupata Ofisi ya kudumu baada ya kupewa jengo lililokuwa likitumiwa na iliyokuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati katika eneo la Forodhani. Vikao vinne (4) vya Baraza la Madiwani la Jiji vimefanyika na kujadili namna bora ya utendaji kazi wa pamoja kati ya Jiji na Manispaa zilizopo katika Mkoa wa Mjini Magharibi; mapungufu yaliyopo kwenye Sheria Nambari 07/2014 Sheria ya Serikali za Mitaa inayopelekea ugumu wa uwepo wa Jiji na Manispaa katika eneo moja pamoja na kujadili mipango ya bajeti ya jiji. Jiji limeendesha kikao cha mashirikiano kilichowahusisha watendaji wakuu na Manispaa za Mkoa wa Mjini Magharibi kujadili masuala ya usafi, masoko na ukusanyaji mapato. Kadhalika Madiwani walipatiwa semina ya mafunzo elekezi kuhusiana na miongozo ya uendeshaji wa Serikali za Mitaa. Aidha, shughuli za uendeshaji ikiwemo ununuzi wa vitendea kazi matengenezo ya jengo la Afisi na samani yamefanyika.

**BARAZA LA MANISPAA MJINI**

**91.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza la Manispaa Mjini lilipanga kuimarisha usafi wa Mji, kuimarisha huduma za kijamii, kusimamia huduma za sekta zilizogatuliwa na kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia za kieletroniki.

**92.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha usafi wa mji unaimarika, Baraza limebinafsisha huduma za usafi kwa kampuni ya *Green Waste Pro* ambayo imeanza kufanya kazi tarehe 15/12/2020 katika zoni ya Mji Mkongwe na zoni ya Magharibi ikihusisha maeneo ya Makadara, Saateni, Mwembeladu, Rahaleo, Kwahani, Kikwajuni na Miembeni. Maeneo mengine yaliyobaki huduma za usafi zinaendelea kutolewa na Baraza la Manispaa Mjini. Shughuli za uhamasishaji jamii juu ya usafi wa mazingira zimeendelea

kutolewa kupitia vyombo vya habari na mikutano ya Shehia ambapo vipindi 38 na matangazo 20 yamerushwa hewani sambamba na kutoa elimu kupitia gari ya matangazo. Aidha, ndoo za kuwekea taka 525 zimetolewa katika maeneo mbali mbali ya Manispaa pamoja na kufanya mazoezi maalum ya usafi kwa kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa wiki kwa kushirikiana na Idara Maalum za SMZ, wananchi wa maeneo husika pamoja na Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali.

93. **Mheshimiwa Spika,** katika kuleta haiba ya mji, Baraza la Manispaa Mjini chini ya Mradi unaofadhiliwa na Jiji la Posterdam la Ujerumani limeendelea na ujenzi wa bustani ya Migombani (Botanic Garden) kwa kujenga kiwanja cha mpira wa kikapu, eneo la kufurahishia watoto, uwekaji wa taa 15, ujenzi wa kibanda cha Mfumo wa umeme wa jua, kuotesha miti 1,435 ya matunda na maua pamoja na kutengeneza bwawa la samaki. Aidha, Baraza limeendelea na uimarishaji wa maeneo mapya ya bustani yakiwemo Kilimani, Migombani, Mnazi mmoja na Mlandege. Vile vile, matengenezo ya taa za mitaani na taa za barabarani yanaendelea kufanyika katika maeneo ya Mji Mkongwe, Kwa Mchina Mwanzo (Kwerekwe) na Mkunazini kwa ubadilishaji wa nyaya, balbu, matengenezo ya nguzo pamoja na kuendelea na matengenezo ya taa mbovu za barabarani.

94. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha huduma ya mama na mtoto jumla ya watoto 35,910 wamepatiwa chanjo ya *penta 3*, watoto wa kike 341 wamepatiwa chanjo ya kwanza na ya pili ya pepo punda na watoto 70 wamepatiwa chanjo ya Saratani ya Mlango wa Kizazi na Wanafunzi 232 wa skuli ya maandalizi Kidutani wamefanyiwa upimaji wa afya kwa magonjwa ya meno, macho, pua na koo. Huduma ya kuangalia maendeleo ya ukuwaji wa mtoto tumboni (*Ultra Sound*) imeendelea kufanyika kwa kinamama waja wazito 4,301 katika Hospitali za (Mpendae 1,856, Sebleni 1,297 na Chumbuni 1,148) ambapo kina mama 121 wamepewa rufaa ya kwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa uchunguzi na matibabu zaidi. Aidha, kina mama 1,110 wamejifungulia katika vituo vya afya na hakukuwa na kifo cha mama na mtoto kilichoripotiwa.

95. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa elimu ya maandalizi na msingi, Baraza lilifanya uhamasishaji na uandikishaji wa wanafunzi wapya ambapo hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya wanafunzi 6,537 wakiwemo wa maandalizi 1,967 (wanaume 969 na wanawake 998) na Msingi jumla ya wanafunzi 4,570 (wanawaume 2,261 na wanawake 2,309) sawa na asilimia 94 kati ya wanafunzi 2,100 waliokadiriwa kuandikishwa. Wanafunzi 4,570 wa darasa la kwanza wameandikishwa kati ya wanafunzi 3,800 waliokadiriwa kuandikishwa sawa na asilimia 120. Aidha, matengenezo ya madarasa manne ya skuli ya Mwembemakumbi yamefanyika kwa ujenzi wa sakafu, ukuta, na upakaji wa rangi. Vile vile, matengenezo ya vyoo katika skuli ya Mwembeshauri yamefanyika sambamba na upakaji rangi wa mbao za kuandikia kwa skuli zote za maandalizi na msingi.

**BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "A"**

96. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza la Manispaa Magharibi "A" limepanga kuimarisha usafi wa Miji na maeneo ya kazi, kuimarisha utoaji wa huduma za kijamii, kuimarisha ukusanyaji wa Mapato na kutoa huduma za kiutendaji.

97. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha usafi wa mazingira, Baraza la Manispaa Magharibi "A" limefanya ukaguzi wa usafi kwa nyumba 33,456 katika Shehia zote 31 na kugundua nyumba 738 hazikua na karo za kuhifadhia maji machafu. Zoezi la ukaguzi kwa wafanyabiashara 6,396 lilifanyika kwa (vioski 1479, migahawa 650, mabucha 441, bekari 79, maduka ya chakula 2985 na mama/baba lishe 762) ambapo wafanya biashara 180 walikutwa na makosa ya kutozingatia kanuni za usafi kwenye biashara zao. Hivyo, Baraza lilitoa muda wa wiki mbili kwa wahusika wote kurekebisha kasoro zilizobainishwa. Vile vile, Baraza limeendesha zoezi maalum la kuondosha taka katika majaa yasiyo rasmi ambapo jumla ya tani 29,556 zimezolewa.

98. **Mheshimiwa Spika,** jitihada za kuimarisha huduma za afya ya msingi, Baraza limenunua na kusambaza vifaa tiba katika vituo vyote 13 vya Afya. Huduma za mama na mtoto zimeendelea kutolewa ambapo kina Mama wajawazito 927 walijifungua katika vituo vya afya, 1,220 walipatiwa

huduma za uchunguzi wa dalili za hatari zinazoambatana na ujauzito na watoto 18,784 walipatiwa chanjo za maradhi ya Surua, Kifua Kikuu, Polio na Dondakoo pamoja na kutoa vyandarua 7,524 kwa wananchi. Aidha, wananchi 12,293 walipewa ushauri nasaha na kuchunguzwa Virusi vya UKIMWI ambapo kati ya hao wananchi 54 waligundulika kuwa na Virusi vya UKIMWI.

99. **Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa Madarasa matano (5) mapya mawili (2) skuli ya Chunga na matatu (3) skuli ya Dole na ukarabati wa vyoo katika skuli za Kizimbani, Mtopepo na skuli ya Dole umefanyika. Aidha, madawati 380 yamepokelewa na kusambazwa katika skuli 11.Kwa upande wa sekta ya elimu, Baraza la Manispaa limeandikisha wanafunzi 7,225 wakiwemo Maandalizi 2,950 (wanaume 1,025 na wanawake 1,925) na Msingi 4,275 (wanaume 2021 na wanawake 2,254) ukilinganisha na wanafunzi 12,345 walioandikishwa 2019. Aidha, watoto 6,128 wamepatiwa lishe katika skuli 24 na vituo 24 vya TUTU na Walimu 123 wa somo la Hisabati wa Darasa la tatu na Darasa la nne (4) walijengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo juu ya mbinu bora za kufundishia.

100. **Mheshimiwa Spika,** Baraza limeendelea kuimarisha huduma za kilimo na utunzaji wa mazingira ambapo miche 85,246 imeatikwa kati ya miche 100,000 iliyotarajiwa kuatikwa katika kitalu cha Selemu, Mfenesini na Mwera. Kati ya miche hiyo, miche 4,702 minazi, miche 80,094 misitu, viungo, na matunda na miche 450 ya Bustani. Kwa upande wa kilimo cha Mpunga kinachotegemea mvua, shughuli za uchimbaji na uburugaji katika mabonde 13 yenye ukubwa wa ekari 1,107.5 zimefanyika ambapo ekari 787.75 zimechimbwa na ekari 741.25 zimeburugwa na ekari 741 za mpunga zimepandwa. Mavuno ya kilimo cha mpunga wa umwagiliaji katika msimu mdogo wa vuli ulipanda kufikia tani 4.51 kutoka tani 4.4 kwa hekta. Kwa upande wa mifugo, ng'ombe 542 wametibiwa, mbwa 706 na paka 102 wamepatiwa chanjo ya maradhi ya kimeta. Aidha, mikoko 5,500 imepandwa katika Shehia ya Chuini kudhibiti maji ya bahari kuja maeneo ya kilimo.

101. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa masuala mtambuka, Wajumbe 53 wa kamati za Mazingira na Shehia wamepatiwa mafunzo ya mazingira na

mabadiliko tabianchi katika Shehia zote 31 za Wilaya ya Magharibi “A” kwa lengo la kuimarisha uhifadhi bora wa Mazingira na kuimarisha uelewa juu ya Mabadiliko ya Tabianchi. Vikundi sita (6) vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vimefikiwa pamoja na vijana 120 wamehamasishwa juu ya upatikanwaji wa fursa mbalimbali kwa lengo la kuwawekea mazingira wezeshi ya upatikanaji wa misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Zoezi la utoaji wa misaada ya vyakula kwa makundi maalum na waathirika 81 wa maafa lilifanyika kwa lengo la kuwafariji na kuwapunguzia ukali wa maisha waathirika hao.

**102. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ustawi wa wafanyakazi na Waheshimiwa Madiwani, Baraza limewalipa stahiki Waheshimiwa Madiwani 22 na wafanyakazi 1,461, limewapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wawili (Shahada ya pili katika fani ya Uchumi na Fedha na Stashahada katika fani ya Uhasibu). Aidha, mafunzo ya sera, sheria na miongozo kwa watendaji yametolewa ikiwemo Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011, Sheria Nam 7/2014 ya Serikali za Mitaa, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, katiba ya Zanzibar na Muongozo wa Mabaraza ya Wadi na Shehia.

**BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI “B”**

**103. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza la Manispaa Magharibi 'B' lilipanga kuimarisha usafi wa Mji, kuimarisha huduma za kijamii, kusimamia huduma za kisekta na kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia za kieletroniki.

**104. Mheshimiwa Spika,** Baraza limechukua jitihada za kuimarisha usafi wa mazingira kwa kufanya usafi katika maeneo ya barabara, kusafisha mitaro ya maji ya mvua na kutoa elimu ya usafi wa mazingira katika Shehia kupitia mikutano na vyombo vya habari. Baraza lilikadiria kuzoa tani 7,209 za taka na kufanikiwa kuzoa tani 7,105 sawa na asilimia 99. Vile vile, lilifanya zoezi la uondoshaji wa majaa yasio rasmi katika maeneo ya Magogoni, Kijitoupele, Chukwani, Pangawe, Taveta, Mombasa, Magereza, Mwanakwerekwe, Kwarara, Uzi, Kwamchina, Tomondo na Melinne. Ofisi imefanya jitihada za kuimarisha Bustani za Kiembe samaki, Mombasa na

Mwanakwerekwe kwa lengo la kuleta haiba nzuri katika maeneo ya Manispaa.

105. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza miradi na utoaji huduma za maendeleo kwa Wananchi, Barazalimejenga njia ya wapitao kwa miguu pembezoni mwa barabara ya Uwanja wa ndege wa Zanzibar kwa wastani wa mita za mraba 270 pamoja na matengenezo ya njia za ndani kwa kiwango cha kifusi katika maeneo ya Kisima Mkuyu, Mwanakwerekwe, Jumbi Sokoni, Chukwani, Pangawe na Kwarara pamoja ujenzi wa vivuko katika eneo la Meli nne na Kijitoupele. Vile vile, Baraza limesaidia upatikanaji wahuduma ya maji kwa Wananchi wa Kibondeni kwa kuwawekea miundombinu ya maji ili kuwaondoshea adha ya kukosa huduma hiyo kwa muda mrefu.

106. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa huduma ya Afya, Baraza limeimarisha miundo mbinu ya Afya ambapovituo vitatu vya afya (3) vya (Magogoni, Magirisi na Chukwani)vimefanyiwa matengenezo ikiwemo uwekaji wa miundombinu ya maji na umeme na kufanya ukarabati mkubwa wa kituo cha Afya cha Fuoni kibondeni. Katika huduma za uzazi, jumla ya wajawazito 1,310 walijifungua katika vituo vya Afya vya Manispaa ya Magharibi 'B'na wajawazito 92 walipewa rufaakatika Hospitali ya Mnazimmoja. Kwa upande wa chanjo za watoto za Kifua Kikuu, walengwa walikuwa watoto 6,806 na waliopatiwa chanjo ni 7,165 sawa na asilimia 105. Aidha, chanjo za chini ya miaka mitano *penta 3* walengwa walikuwa watoto 6,485 na waliopatiwa chanjo ni 4,867 sawa na asilimia 75 ya chanjo; na chanjo za mama wajawazito walengwa walikuwa 6,485 na waliopatiwa chanjo ni 2,709 sawa na asilimia 41.7 ya malengo.

107. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa huduma za elimu ya msingi Skuli 27 za maandalizi na Vituo 10 vya TUTU vimepatiwa huduma za uji wa lishe kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wa Maandalizi 6,285kuwa na mazingira rafiki ya kujifunza pamoja na kutoa huduma ya maji na umeme kwa skuli zote za Wilaya ya Magharibi 'B'. Katika kuimarisha kilimo nchini, jumla ya ekari 40.5 za mazao ya chakula na ekari 133 za mazao ya mboga zilipandwa sambamba na kutoa ushauri wa kanuni bora za kilimo ambapo wakulima 784 (Wanawake 289 na wanaume 495) kutoka katika Shehia 18

walinufaika na elimu ya ugani. Aidha, wafugaji 728 walipatiwa ushauri wa upandaji wa malisho, kuchanja mifugo, usafi wa mabanda na mazizi, usafi wakati wa kukama maziwa na utaratibu wa ulishaji pamoja na kuwapatia dawa za minyoo na kinga kwa utaratibu uliopangwa kitaalamu.

**108.Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mkoa wa Mjini Magharibi uliidhinishiwa **Shilingi 35,826,000,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,653,600,000** mishahara, **Shilingi 1,380,500,000** matumizi mengineyo na **Shilingi 32,791,900,000** ni ruzuku za Mabaraza ya Manispaa na Jiji la Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2021, Mkoa uliingiziwa **Shilingi 25,865,184,012** sawa na asilimia **72** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,281,638,745** sawa na asilimia **78** ni mishahara, **Shilingi 302,977,700** sawa na asilimia **22** ni matumizi mengineyo, na **Shilingi 24,280,567,567** sawa na asilimia **74** ni ruzuku za Mabaraza ya Manispaa na Jiji la Zanzibar. Aidha, Mkoa uliidhinishiwa kukusanya **Shilingi 125,000,000** na kukusanya **Shilingi 41,876,000** sawa na asilimia **34**. Kwa upande wa mapato Baraza la Manispaa Mjini liliidhinishiwa kukusanya **Shilingi 5,252,940,000** limekusanya **Shilingi 2,628,343,232** sawa na asilimia **50**, kwa upande wa Baraza la Manispaa Magharibi 'A' lilikadiria kukusanya **Shilingi 1,150,000,000** na limekusanya **Shilingi 929,261,750** sawa na asilimia **81** na Baraza la Manispaa Magharibi B liliidhinishiwa kukusanya **Shilingi 2,150,000,000** na kufanikiwa kukusanya **Shilingi 1,845,817,642** sawa na asilimia **86**.

**MKOA WA KUSINI UNGUJA – FUNGU (D08)**

**109.Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Mkoa wa Kusini Unguja umepanga Kusimamia Shughuli za ulinzi na usalama katika Mkoa; kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto; kusikiliza na kuyapatia ufumbuzi malalamiko na kero za wananchi; kuzipatia Afisi huduma za Utawala na Uendeshaji pamoja na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**PROGRAMU YA KUSIMAMIA SHUGHULI ZA SERIKALI KATIKA MKOA**

**110.Mheshimiwa Spika**, Mkoa umeendelea kusimamia shughuli za Ulinzi na Usalama ili kuhakikisha amani na utulivu inadumishwa. Vikao 47 vya Kamati za Usalama za Mkoa na Wilaya vimefanyika na kuibua mikakati ya usalama ikiwemo kuimarisha doria za nchi kavu na baharini na kuhamasisha mshikamano wa wananchi katika jamii. Mikakati hiyo imepelekea kuimarika hali ya amani na utulivu katika kipindi cha uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, kuwaunganisha wananchi, sambamba na kukamata matukio sita (6) ya magendo. Aidha, Kamati zimeendelea kuhimiza mashirikiano mema baina ya jamii na wawekezaji katika maeneo ya utalii katika Shehia za Chwaka, Michamvi, Mtende, Bwejuu na Paje jambo ambalo limesaidia kupunguza migogoro kati ya wawekezaji na wanajamii katika Shehia hizo.

**111.Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia maendeleo ya elimu, skuli 75 kati ya 112 zikiwemo 46 za Maandalizi na Msingi na 29 za Sekondari zimefuatiliwa na kubaini baadhi ya wanafunzi kujihusisha na mapenzi pamoja na mashirikiano madogo baina ya wazazi na walimu.Uongozi wa Mkoa umechukua juhudi za kufuatilia mahudhurio na utendaji kazi wa walimu, kudhibiti vitendo vinavyoashiria kudumaza elimu kwa wanafunzi na kuhamasisha jamii kushiriki katika kukuza maendeleo ya elimu ndani ya Mkoa kupitia Kamati za Skuli, vikao vya walimu wakuu na Kongamano la elimu.

**112.Mheshimiwa Spika,** katika kuratibu upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama, Mkoa unapata huduma ya maji kwa wastani wa asilimia 70 ya mahitaji. Miongoni mwa Shehia ambazo zinakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji ni Cheju, Kikungwi, Uzi, Kitogani, Bambi, Ndijani Mseweni, Michamvi na Bwejuu. Mkoa umefuatilia utatuzi wa changamoto hiyo na kuratibu matengenezo ya miundombinu ya maji katika Shehia za Bambi, Ndijani Mseweni, Michamvi na Bwejuu. Aidha, kupitia washirika wa maendeleo, visima vitano (5) vimechimbwa katika Shehia ya Kajengwa, Tasani, Muyuni, Kijini na Ghana na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

**113.Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza dhana ya Uchumi wa Buluu, Mkoa umewahimiza wananchi kutumia rasilimali ya bahari bila kuathiri mazingira yake, kuvua kwa kutumia uvuvi wa kisasa ili kulinda mazingira

wakati wote wanapokua katika shughuli za uvuvi na kilimo cha mwani. Wakulima 60 wa mwani na Kamati za Uvuvi 10 za Shehia ya Chwaka, Marumbi, Uzi Ng'ambwa, Unguja Ukuu Kaepwani, Mtende, Mzuri, Tasani, Kizimkazi Mkunguni, Michamvi na Kitogani zimefikiwa. Kupitia uhamasishaji huo baadhi ya Shehia zimeitikia wito wa kutunza mazingira mfano Shehia ya Michamvi imepanda majaniaina ya*"Mla Kasa"*na Shehia za Unguja Ukuu Kaepwani na Kitogani zimepanda mikoko kwa lengo la kuzuia mmomonyoko wa fukwe na kuongeza haiba nzuri pembezoni mwa bahari.

**114.Mheshimiwa Spika,** Mkoa umefatilia miradi minane (8) ya maendeleo inayotekelezwa kupitia sekta mbalimbali katika Mkoa wa Kusini Unguja. Miradi yenyewe ni ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu, Nyumba ya Kurekebisha tabia kwa waathirika wa dawa za kulevya, Skuli ya Sekondari Kibuteni (Hasnuu Makame), Chuo cha Mafunzo ya Amali Makunduchi, barabara ya Charawe – Ukongoroni – Bwejuu (23.3km), Hospitali ya Rufaa - Binguni, Jaa la Kisasa Kibele na Kilimo cha Umwagiliaji maji katika bonde la Cheju. Miradi miwili (2) ya Skuli ya Sekondari Kibuteni (Hasnuu Makame) na Jaa la Kisasa Kibele imekamilika na imeanza kutoa huduma kwa wananchi na miradi sita (6) iliyobakia utekelezaji wake unaendelea.

**115.Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2020/2021 matukio 96 ya udhalilishaji yameripotiwa ilikilinganishwa na matukio 79 kwa mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia 16. Ongezeko hili linatokana na mwamko wa jamii katika kuripoti matukio ya udhalilishaji wa wanawake na watoto. Kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF), Mkoa umeratibu utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kupambana na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017 – 2022. Vikao 36 vya waratibu wa wanawake na watoto katika shehia na kamati za kupambana na vitendo vya udhalilishaji za Wilaya vimefanyika kujadili mikakati ya kupunguza vitendo hivyo. Baadhi ya mikakati iliyotekelezwa ni utoaji wa elimu kwa umma kupitia Redio Jamii za Wilaya ya Kati na Kusini ambapo wananchi wameaswa kutokuwa na muhali kwa wahalifu wa vitendo hivyo.

**PROGRAMU YA UTAWALA NA UENDESHAJI**

**116. Mheshimiwa Spika,** Mkoa umefanya ziara ya kuwakagua watu wenye ulemavu 91 katika Shehia 13 za Dunga Kiembeni, Dunga Bweni, Kidimni, Bambi, Binguni, Uzi Ng'ambwa, Kizimkazi, Makunduchi, Paje, Kitogani, Muungoni, Michamvi, Kibuteni na Muyuni A, B na C. Kufuatia ziara hizo watu wenye ulemavu 28 kati yao Wilaya ya Kusini 19 na Wilaya ya Kati 9 wamepatiwa msaada wa mavazi na vikundi vinne vijuulikanavyo kwa majina ya "*Jipe Moyo*", *"Juhudi Mbele"*,*"Yajayo Yanafurahisha"*na *"Umoja ni Nguvu"*vimepatiwa maelekezo ya uendeshaji wa shughuli zao pamoja na kutakiwa kujisajili. Aidha, msaada wa Shilingi 5,000 kwa wananchi wanye mazingira magumu 519 umetolewa ukilinganishwa na wananchi 603 waliopatiwa msaada huo mwaka 2019/2020. Upungufu huo umetokana na baadhi ya wananchi hao kufariki dunia na wengine kufikia umri wa miaka 70 ambao wameingizwa katika mfuko wa Pencheni Jamii.

**117. Mheshimiwa Spika,** Mkoa umeendelea kujenga mazingira mazuri na salama ya kufanyia kazi kwa kuipatia Afisi vitendea kazi na kuwapatia stahiki zao watumishi. Wafanyakazi watano (5) wameendelea kujengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani za Mipango ya maendeleo Vijijini; Uchumi na Fedha; Utawala wa Umma; Uongozi wa Biashara na Utunzaji wa Kumbukumbu.

**PROGRAMU YA USIMAMIZI WA SERIKALI ZA MITAA**

**BARAZA LA MJI KATI**

**118. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021,Baraza la Mji Kati limeimarisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi kwa kuendeleza miradi ya maendeleo ikiwemo, uchimbaji wa visima vinne (4) katika Shehia za Umbuji, Dunga Bweni na Ghana; kufanya matengenezo madogo madogo ya vituo sita (6) vya Afya vya Mpapa, Tunguu, Mchangani, Miwani, Ndijani Mseweni na Dunga. Aidha, madarasa mawili ya Skuli ya Maandalizi Uchukuni yameezekwa na skuli ya msingi Mchangani imefanyiwa matengenezo madogo madogo. Vile vile, Baraza limefanya mapitio kwa Kamati za Mashauriano ya Shehia na Mabaraza ya Wadi ambayo yanaendelea kufanya kazi ya kuwahudumia wananchi.

**119. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza usafi wa maeneo na miji midogo, Baraza limeendeleza kuzoa taka katika maeneo hayo ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 limepanga kuzoa tani 3,044 na limefanikiwa kuzoa tani 2,088 sawa na asilimia 68 kulinganisha na tani 5,050 sawa na asilimia 65 ya taka zilizozolewa kwa mwaka 2019/2020. Upungufu huu umetokana na uchache wa vitendea kazi vikiwemo gari za kuzolea taka. Vile vile, Baraza limesambaza madoo ya kuzolea taka 45 katika maeneo mbalimbali yakiwemo Mji mdogo wa Dunga kibaoni, Mji wa Tunguu, Koani kwa kozi, Jumbi na Kidimni kwa lengo la kuwezesha uchukuaji wa taka. Aidha, zoezi la usafi la kila Jumamosi ya kila wiki limeendelea ndani ya Wilaya.

**120. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa masuala mtambuka, Baraza limeshirikiana na Jumuiya ya 'Zanzibar Mama' kutoa misaada ya nguo na vyakula kwa wananchi 483 katika shehia 12 wakiwemo wananchi 258 wenye ulemavu na mazingira magumu, yatima na vikundi vya wanawake pamoja na kujenga nyumba yenye chumba kimoja ya mwananchi mwenye mazingira magumu. Vilevile, elimu ya ujasiriamali, udhalilishaji, dawa za kulevya, VVU na UKIMWI kwa vijana 234 imetolewa ili kupunguza maambukizi mapya ya VVU na utumiaji wa dawa za kulevya. Aidha, kikao kimoja (1) cha Kamati ya Kitaalamu ya Maafa kimefanyika kujadili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya mvua ikiwemo mafuriko na maradhi ya miripuko, pamoja na kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira kwa Shehia 42 na kupitia redio jamii KATI FM.

**121. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza sekta ya kilimo, wakulima 1,559; wafugaji 918; wavuvi 100 wa samaki pamoja na kikundi kimoja (1) cha uvuvi wamepatiwa Elimu ya Ugani kwa lengo la kuwawezesha kufuga na kulima kilimo cha kisasa chenye tija. Ekari 1,686.25 za mpunga wa kutegemea mvua na ekari 339.9 za kilimo cha umwagiliaji maji zimevunwa, ekari 743 zimechimbwa na ekari 500.75 zimeburugwa ikiwa ni maandalizi ya kilimo cha mpunga kwa msimu wa mvua 2020/2021. Aidha, Baraza limefanya utafiti wa kupe kwa ng'ombe 122 katika Shehia za Binguni, Bungi, Ndijani, Cheju na Unguja Ukuu sambamba na kutoa chanjo kwa

mifugo 1,673 kati ya 1,500 sawa na ongezeko la asilimia 11 ya lengo iliyojipangia.

122. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Mji Kati limeendelea kuimarisha huduma katika vituo vya afya, zikiwemo upatikanaji wa vifaa vya usafi, vifaa tiba, vitendanishi, maji na umeme kwa vituo vyote 27. Baraza lilipanga kutoa chanjo ya Saratani ya shingo ya mlango wa kizazi kwa watoto wa kike 2,000 na kufanikiwa kutoa chanjo kwa watoto 765 wenye Umri wa miaka 9-14 sawa na asilimia 38.3. Mama Wajawazito 387 wamejifungulia katika Vituo vya Afya ambapo 14 wamepatiwa rufaa. Baraza limefanikiwa kusogeza huduma ya afya karibu na jamii kupitia programu ya Afya ya Kijiji kwa kuzikutanisha Shehia 42 za Wilaya ya Kati kwa lengo la kubaini matatizo ya kiafya yanayowakabili na kuyapatia tiba na ushauri unaostahiki. Katika kupambana na ugonjwa wa malaria, kesi 133 za Malaria zimegundulika ikiwemo watu wazima 122 na watoto11 walifanyiwa uchunguzi na kupatiwa tiba.

123. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utoaji wa elimu ya maandalizi na msingi, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Mji Kati limepanga kuandikisha wanafunzi wa maandalizi 2,500 na kufanikiwa kuandikisha wanafunzi 2,203 (wanawake 1,072 na wanaume 1,131) sawa na asilimia 88 na kwa upande wa msingi, Baraza lilipanga kuandikisha wanafunzi 4,000 na kufanikiwa kuandikisha wanafunzi 3,802 (wanawake 1,795 na wanaume 2,007) sawa na asilimia 95. Aidha, nauli kwa walimu 437 zimelipwa pamoja na usambazaji wa lishe kwa skuli 44 za maandalizi kwa kipindi cha miezi ya Oktoba, Febuari na Machi umefanyika.

124. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi, wafanyakazi 140 wamepatiwa stahiki zao ikiwemo posho la likizo 58, gharama za mazishi saba (7), malipo baada ya saa za kazi sita (6) posho maalum 16, mafunzo ya Sheria ya Utumishi na usalama kazini 20, mafunzo elekezi 33 na mtumishi mmoja amelipiwa gharama za mafunzo ya mda mrefu katika fani ya Rasilimali watu ngazi ya Stashahada sambamba na upatikanaji wa vitendea kazi ili kuongeza ufanisi kwa utoaji huduma. Vile vile, vikao 14 vimefanyika vikiwemo vikao vya Baraza la Madiwani, Kamati Tendaji, Kamati za kudumu, Kamati ya Ukaguzi na

Kamati ya Uongozi kwa lengo la kupanga na kutekeleza mikakati ya kuleta maendeleo ikiwemo kuimarisha usafi wa mazingira, kuongeza ukusanyaji wa mapato, matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji mapato, kuboresha huduma za jamii pamoja na miradi ya maendeleo kwa jamii.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI**

**125.Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha usafi wa mazingira, Halmashauri ilipanga kuzoa tani 2,530 za taka na imefanikiwa kuzoa tani 2,103 sawa na asilimia 83. Zoezi la kufanya usafi wa mazingira kila mwisho wa wiki linaendelea ambapo Shehia sita (6) za Kitogani, Michamvi, Paje, Jambiani, Kiongoni na Bwejuu zimewekewa kipaumbele kutokana na kutembelewa na wageni mara kwa mara. Juhudi za makusudi zimechukuliwa kuondosha majaa yasiyo rasmi kwenye shehia hizo pamoja na kukamilisha taratibu za kubinafsisha suala la uzoaji taka kwa sekta binafsi. Vile vile, mikakati ya kuhamasisha jamii kufunika mashimo ya vyoo na kutoa elimu ya kuimarisha usafi wa mazingira zimetolewa.

**126.Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa miradi ya wadi, Halmashauri ilipanga kukamilisha ujezi wa nyumba ya Daktari ya familia mbili katika kituo cha afya Kajengwa na kufanikiwa kukamilisha upande mmoja wa nyumba hiyo. Vile vile kwa kushirikiana na Benki ya CRDB na mfuko wa maendeleo ya Mbunge wa Jimbo la Makunduchi, Halmashauri imekamilisha Jengo la kusubiria wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Makunduchi ambalo tayari linatumika.

**127.Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha watoto wanapatiwa elimu ya maandalizi na msingi, Halmashauri imeandikisha wanafunzi 2,722 wa maandalizi na msingi kwa mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia tisa (9) ya wanafunzi 2,486 walioandikishwa mwaka 2019/2020. Kati yao maandalizi 1,338 (wanaume 664, wanawake 674) na msingi 1,434 (wanaume 581 na wanawake 853). Aidha, Halmashauri imetoa nauli kwa walimu 146 na huduma ya lishe kwa skuli zote 16 za maandalizi kwa mwezi wa Disemba, 2020 na Febuari, 2021. Vilevile Afisi imefanya ziara za kukagua skuli 10 zikiwemo Michamvi Maandalizi na Msingi, Bwejuu Maandalizi na Msingi, Paje Msingi, Jambiani Maandalizi na Msingi,

Kikadini, Kizimkazi Dimbani Maandalizi, Muyuni, Kibuteni na Kitogani na kuzipatia ufumbuzi changamoto za walimu zikiwemo masula ya likizo, nauli, uthibitisho wa kazi na marekebisho ya mishahara.

**128.Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa huduma za afya ya msingi, Wagonjwa 51,626 wamepatiwa huduma katika vituo vya Afya 12 vilivyopo Wilaya ya kusini kati yao 16,249 ni watoto wenye umri chini ya miaka mitano na 35,377 wenye umri wa kuanzia miaka mitano na kuendelea. Wagonjwa hao walichunguzwa na kutibiwa maradhi tofauti yakiwemo Malaria, Kuharisha, Shindikizo la damu na Kisukari. Huduma za mama na mtoto, zimeendelea kutolewa kwa mama wajawazito 1,360 waliohudhuria Kliniki kuchunguzwa matatizo mbalimbali pamoja na kuangalia maendeleo ya mtoto. Aidha mama wajawazito 902 wameripotiwa kujifungulia vituoni. Vile vile, Halmashauri imetoa chanjo kwa watoto 6,928 kati ya watoto 6,645 waliokadiriwa sawa na asilimia 104 ili kuwakinga watoto na magonjwa mbali mbali.

**129.Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya kilimo, Halmashauri imeotesha miche 24,252 ikiwemo minazi 3,000 kati ya miche 50,000 iliyotarajiwa kuoteshwa sawa na asilimia 49. Asali tani tatu (3) zenye thamani ya Shilingi 128,700,000 na mwani tani 385 wenye thamani ya shilling 461,400,000 zimevunwa. Aidha, wafugaji 1,107 wamepatiwa elimu ya ufugaji na namna ya kuipatia kinga mifugo yao jambo lililopelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa kutoka lita 4.5 mwaka 2019/2020 hadi lita 5.5 mwaka 2020/2021 kwa ng'ombe mmoja. Vilevile wakulima 800 wametembelewa na kupatiwa ushauri wa kitaalamu ambao umepelekea kuongezeka kwa mazao ya mboga mboga. Afisi kwa kushirikiana na benki ya NMB imewapatia wavuvi 150 mafunzo ya kuwezesha kupatiwa mikopo na kuwekeza katika uchumi wa buluu.

**130.Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini imeimarisha huduma za kiofisi, kwa kuwapatia stahiki zao watumishi 155 wakiwemo 118 wamepatiwa likizo, 15 wamepatiwa mafunzo elekezi (Induction Course), 10 wamepatiwa mafunzo ya kuwapima watumishi (Performance Appraisal), wawili (2) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani ya Rasilimali watu ngazi ya Shahada ya Kwanza na watumishi 10 wamelipwa malipo ya

muda wa ziada. Vile vile, Afisi imeongeza vitendea kazi na upatikanaji wa huduma ili kuongeza ufanisi na weledi katika kazi.

131. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mkoa wa Kusini Unguja, uliidhinishiwa **Shilingi 14,068,800,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,369,900,000** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 758,630,000** matumizi mengineyo na **Shilingi 11,940,270,000** ni ruzuku za Baraza la Mji Kati na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini. Hadi kufikia Machi, 2021 Mkoa umeingiziwa **Shilingi 9,468,117,987** sawa na asilimia **67**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,100,369,402** sawa na asilimia **80** ni mishahara, **Shilingi 160,149,743** sawa na asilimia **21** Matumizi mengineyo na **Shilingi 8,207,598,842** sawa na asilimia **69** ni ruzuku. Aidha Mkoa umepangiwa kukusanya mapato ya **Shilingi 50,750,000** kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina na hadi kufikia Machi, 2021 Mkoa umekusanya **Shilingi 24,539,000** sawa na asilimia **48**. Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza la Mji Kati lilidhinishiwa kukusanya **Shilingi 1,200,000,000** na limefanikiwa kukusanya **Shilingi 875,694,309** sawa na asilimia **73** na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini iliidhinishiwa kukusanya **Shilingi 550,612,000** na kufanikiwa kukusanya **Shilingi 392,896**,925 sawa na asilimia **71**.

**MKOA WA KASKAZINI UNGUJA - (D09)**

**PROGRAMU YA KUSIMAMIA SHUGHULI ZA SERIKALI KATIKA MKOA**

132. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza programuya Kusimamia shughuli za Serikali, Mkoa umesimamia hali ya ulinzi na usalama kwa kufanya vikao 48 vya Kamati za Usalama ambavyo vimepelekea kufanyika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kwa amani na utulivu pamoja na kuratibiwa kwa ufanisi ziara zilizofanywa na viongozi wakuu wa kitaifa. Mkakati wa kukabiliana na uhalifu katika Mkoa umeandaliwa ikiwemo utambuzi wa viashiria vya uvunjifu wa amani pamoja na kuundwa vikosi kazi vitatu vya kukabiliana na matukio ya uhalifu ambapo gari tatu za wizi wa mchanga, boti mbili na vifaa vya uvuvi haramu, wahamiaji haramu 32, madada poa wanane, mashua mbili zinazojihusisha na usafirishaji wa magendo pamoja na vijana

wanaojihusisha na dawa za kulevya vimekamatwa na kufikisha mbele ya vyombo vya sheria.

**133. Mheshimiwa Spika,** Mkoa umefanya ziara 16 za kusikiliza kero katika Shehia 31 zilizopelekea kutatuliwa changamoto za maji katika Shehia nne za Fukuchani, Nungwi, Kitope na Kidombo pamoja na utatuzi wa changamoto ya umeme katika Shehia nne za Mahonda, Kitope, Mgambo na Mkwajuni. Aidha, Mkoa umepokea na kusikiliza malalamiko 1,221 ya wananchi ambayo malalamiko 603 yametatuliwa kwa wananchi kusaidiwa matibabu, usafiri, ada na vifaa vya masomo pamoja na mahitaji ya kujikimu kimaisha. Mkoa umefuatilia na kutatua migogoro ya Ardhi ambapo jumla ya migogoro 191 ya Ardhi imeripotiwa (149 Wilaya Kaskazini 'A', na 42 Wilaya ya Kaskazini 'B'). Kati yao migogoro 20 imetatuliwa na 171 ipo katika hatua za utatuzi kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi.

**134. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha na kukuza shughuli za kiuchumi, Mkoa umeratibu kutengwa kwa maeneo ya viwanda ambayo ni Mahonda hekta 137 na Nungwi hekta tano, umeratibu shughuli za uwekezaji wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa katika eneo la Fungurefu na umeratibu kurejea huduma za kuruka na kutua ndege za ndani katika Kiwanja cha Ndege Kigunda. Mradi wa umwagiliaji maji wenye ukubwa wa hekta 486 ambapo mabwawa mawili yameshakamilika ikihusisha misingi ya visima viwili pamoja na kuwaunganisha wavuvi na benki ili waweze kupata mikopo itakayo wawezesha kununua boti na zana za kisasa. Aidha, Mkoa umefanya maandalizi ya tamasha la vyakula vya mazao ya baharini (Zanzibar sea food festival) ambalo lina lengo la kuwainua kiuchumi wavuvi na wajasiriamali wa Mkoa kwa kuwaunganisha na wawekezaji wa hoteli za Kitalii.

**135. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha masuala ya huduma za kijamii, Mkoa umefanya harambee ya kuchangia ujenzi wa kituo cha Afya cha Kidagoni ambapo **Shilingi 37,000,000** zimechangiwa ikiwa **Shilingi 27,000,000** ni fedha taslim na **Shilingi 10,000,000** ni vifaa vya ujenzi. Katika kukabiliana na upungufu wa damu, mabonanza mawili ya uchangiaji damu yamefanyika katika hospitali ya Wilaya Kivunge ambapo jumla ya unit 965 za damu zimepatikana (401 Wilaya ya Kaskazini 'A' na 564 Wilaya ya Kaskazini 'B')

ikiwa ni ongezeko la unit 345 ikilinganishwa na mabonanza yaliyofanyika mwaka 2019/2020. Aidha vifaa vya Hospitali ikiwemo dawa, vifaa tiba, mitungi ya gesi, tray za kubebea maiti vilitolewa ili kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

**136.Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa elimu, Mkoa umehakikisha walimu wanaoishi nje ya Mkoa wanafika skuli mapema na kuanza kufundisha kwa wakati. Njia mbadala iliyotumiwa katika kuondoa tatizo la uchelewaji wa walimu ni kufanya vikao na wamiliki wa gari za abiria ili waweze kutoa unafuu wa nauli kwa walimu wakati wa kwenda na kurudi skuli. Kupitia vikao hivyo wamiliki wa gari za abiria wamekubali kuwatoza walimu nauli ya Shilingi 1,000 popote pale anaposhuka wakati wa kwenda au kurudi skuli kwa Wilaya ya Kaskazini 'A' na kwa upande wa Wilaya ya Kaskazini 'B' juhudi zinaendelea. Hali hii imepelekea walimu kuwahi kufika skuli kwa wakati na hivyo kuondoa uwezekano wa walimu kutokukamilisha mtaala wa masomo kwa wakati. Kadhalika katika kupunguza tatizo la upungufu wa madarasa, Mkoa umeratibu maandalizi ya tamasha la vyakula vya mazao ya baharini ambapo fedha zote zitakazopatikana kupitia tamasha hilo zitatumika kujenga madarasa yasiyopungua 150. Aidha, Mkoa umeratibu upatikanaji wa mchanga kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la skuli ya Donge Sekondari ambapo jumla gari 26 za tani 10 zilichangiwa na Serikali ya Mkoa.

**137.Mheshimiwa Spika,** Mkoa umeratibu ziara za viongozi wakuu wa Kitaifa kwa mafanikio makubwa kupitia utekelezaji wa baadhi ya maagizo na ahadi zao wakati wakitembelea maeneo mbali mbali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja kukagua shughuli za maendeleo na kusikiliza kero za wananchi. Katika ziara ya kutembelea kijiji cha Kipandoni, Mheshimiwa Makamu wa pili wa Rais aliagiza kutengenezwe barabara; Kibumbwi aliagiza upelekaji wa maji, umeme, skuli na ujenzi wa barabara inayoelekea kijiji hicho. Maagizo hayo yametekelezwa kwa kujengwa barabara yenye urefu wa Kilomita mbili (2km) kwa kiwango cha kifusi, umeme umeshafikishwa, usambazaji wa maji umeshakamilika na maji yameshaanza kutumika na skuli imebakia hatua utiaji wa milango na upakaji wa rangi ili iweze kuanza kutumika.

**138.Mheshimiwa Spika,** Maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar alipotembelea kiwanda cha Sukari Mahonda yameanza kutekelezwa kwa kuhakikisha wananchi wanaofanyakazi katika kiwanda hicho wanapatiwa haki zao kwa mujibu wa sheria na wananchi wamehamasika kulima kilimo cha miwa ili kunufaika na uwepo wa kiwanda hicho.Jumla yawakulima wa zao la miwa 220 kati ya 320 waliokuwa na madai katika kiwanda cha sukari wameshalipwa jumla ya **Shilingi 160,000,000** na waliobakia watalipwa kwa awamu ya pili. Kadhalika Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa alifika kuzinduwa barabara Matemwe Muyuni iliyojengwa kwa kiwango cha lami. Ziara hizo zimekuwa na manufaa sana kwa wananchi wa Mkoa kwa kupatiwa huduma muhimu za kijamii ikiwemo maji umeme, afya, elimu pamoja na kudumisha tunu za kitaifa kama vile umoja amani na utulivu.

**139.Mheshimiwa Spika,** Mkoa umeendeleza na mapambano dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto kwa kufuatilia kesi za udhalilishaji ambapo hadi kufikia Machi 2021, jumla ya kesi 144 zimeripotiwa. Kati yake, kesi 141 zipo chini ya upelelezi wa polisi; mbili zipo katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na moja ipo mahakamani. Idadi hii ni ongezeko la kesi 29 ya kesi zilizoripotiwa Julai – Machi 2019/2020. Kwa kuwa vitendo hivi vinaongezeka, Mkoa umetoa elimu kwa wananchi 3,397 kupitia mikutano 20 ya hadhara, vipindi vya redio na vipeperushi. Katika kuwarekebisha watoto wanaokinzana na sheria, Mkoa umeanzisha kituo cha marekebisho ya tabia kilichopo ndani ya chuo cha Amali Mkokotoni ambapo walimu 15 wamepatiwa mafunzo ya kusimamia na kuendeleza kituo hicho. Katika kuwahudumia watoto waliotelekezwa na wazazi wao na wale wasiokuwa na walezi, Mkoa umeanzisha mpango wa malezi ya walezi (foster care) ambapo mtoto atalelewa na mlezi aliyekuepo ndani ya jamii badala ya kupelekwa katika vituo vya kulelea watoto.

**PROGRAMU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA MKOA**

**140.Mheshimiwa Spika,** katika program ya utawala na uendeshaji, Mkoa umewapatia wafanyakazi wake stahiki za utumishi kwa mujibu wa sheria wakiwemo wafanyakazi 55 likizo na 17 posho la muda wa ziada na wafanyakazi watatu wamelipiwa ada ya masomo ya muda mrefu. Aidha,

katika kusimamia uwajibikaji wa watumishi Mkoa umefanya ufuatiliaji wa uingiaji na utokaji wa wafanyakazi ofisini ambapo wastani wa mahudhirio kwa mwezi umefikia asilimia 97 kulinganisha na asilimia 67 mwaka 2019/2020. Wafanyakazi 35 wamechukuliwa hatua za kinidhamu ambapo wafanyakazi 30 wamepewa onyo la mdomo na wafanyakazi watano wamepewa onyo la maandishi.

**PROGRAMU YA USIMAMIZI WA SERIKALI ZA MITAA**

**BARAZA LA MJI KASKAZINI 'A'**

**141.Mheshimiwa Spika,** Baraza la Mji Kaskazini 'A' limefanya jitihada mbali mbali katika kusimamia zoezi la usafi wa mazingira katika Wilaya ya Kaskazini 'A'. Jitihada hizo ni pamoja na kufanya operesheni 33 za usafi katika maeneo ya miji, masoko, utalii na uwekezaji ikiwemo Nungwi, Fungurefu, Matemwe, Pwani Mchangani, Gamba, Kinyasini, Mkwajuni na Mkokotoni ambapo jumla ya tani 13,022 zimezolewa. Usafi wa fukwe mita 1,100 umefanyika pamoja na Mitaro zaidi ya kilomita sita imesafishwa; limeongeza upatikanaji wa vifaa vya usafi, kuanzishwa siku maalumu ya usafi na kufanya mikutano ya uhamasishaji jamii kwa maeneo yote. Kutokana na jitihada hizo hali ya usafi imeanza kuimarika ukilinganisha na kipindi kilichopita.

**142.Mheshimiwa Spika,** katika kuchangia maendeleo ya wananchi kupitia mapato ya ndani, Baraza limeendeleza ujenzi wa kituo cha mama na mtoto katika kijiji cha Matemwe, ujenzi wa choo cha matundu mawili katika Soko la Wajasiriliamali Kinyasini, kuendeleza ujenzi wa skuli ya Maandalizi ya Chaani Masingini yenye vyumba vinne vya kusomea, Ofisi mbili za Walimu, matundu sita ya vyoo na ununuzi wa Mashine moja ya maji kwa ajili ya skuli ya Kidagoni ili kupunguza tatizo la upungufu wa maji. Utekelezaji wa shughuli hizi za maendeleo umesaidia kujenga imani kwa wananchi kutokana na kero wanazoziibua kupitia Mabaraza ya Wadi na Kamati za Mashauriano ya Shehia kufanyiwa kazi.

**143.Mheshimiwa Spika,** Baraza la Mji Kaskazini 'A' limefanya uandikishaji wa wanafunzi 9,125 sawa na asilimia 76.7 ya makadirio ya wanafunzi 11,900, ambapo Maandalizi 3,550 (Wanaume 1,325 na Wanwake 2,225) na Msingi 5,575(Wanaume 2721, wanawake 3,054) hii ni ongezeko la wanafunzi 332

ukilinganisha na mwaka 2019/2020 (8,960). Baraza limefanya malipo ya nauli kwa walimu 498 wa skuli za msingi, kulipa posho kwa maafisa elimu watano na wasaidizi wa vituo178 vya TUTU. Aidha, Baraza la Mji limefanya ziara 36 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu katika skuli 31 za Maandalizi na Msingi na vituo vitatu vya TUTU pamoja na kufanya kikao kimoja kilichowashirikisha wasaidizi 174 wa vituo vya TUTU kilichohusu uwajibikaji katika kazi.

**144.Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha afya ya msingi kwa wananchi, Baraza la MjiKaskazini ‘A’ limefanikiwa kufanya uchunguzi wa maradhi mbali mbali kwa wananchi 29,057 ikiwemo upimaji wa mkojo, maradhi ya ngozi, sindikizo la damu, afya meno na kinywa. Jumla ya mama wajawazito 1,311 walihudhuria kliniki na kupatiwa huduma ya vipimo na ushauri elekezi wa kiafya pamoja na kupimwa virusi vya UKIMWI ambapo mama wajawazito watano waligundulika kuambukizwa virusi hivyo. Watoto 1,308 wamepatiwa chanjo kwa ajili ya kuwalinda na kifua kikuu, Pepopunda, Nimonia na Surua. Wananchi 9,692 wamechunguzwa malaria sawa na asilimia 96.6 ya wananchi 10,033 waliokadiriwa ambapo wananchi 240 sawa na asilimia 2.4 waligundulika kuwa na vimelea vya Malaria na kupatiwa matibabu.

**145.Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya kilimo, Baraza la Mji Kaskazini “A” limefanya mikutano ya kutoa elimu ya kilimo cha kisasa katika vijiji vitano ambapo jumla ya wakulima 170 wamefaidika na elimu hiyo. Vilevile, Baraza la mji limefanikiwa kuotesha jumla ya Miche 39,400 ya misitu na matunda (Mikarafuu 27,300, Michungwa 4,800, Milimau 900, Michenza 3,600, Miembe 700, Midimu 300, Mibalungi 100, Miparachichi 400, Mishokishoki 500, Mipapai 800 na miche mingine 1,700) ambayo tayari imeshaanza kutolewa kwa wananchi. Aidha jumla ya wafugaji 40 kutoka shehia za Mkokotoni, Matemwe, Kandwi, Jongowe na Mbuyutende walipatiwa elimu ya chanjo na tiba ya maradhi mbalimbali ikiwemo mahepe na chambavu na jumla ya Wanyama 167 wakiwemo Ng'ombe 152 na mbuzi 15 wamepatiwa tiba.

**146.Mheshimiwa Spika,** katikakuwawezesha wajasiriamali, vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, Baraza la Mji Kaskazini “A” limesaidia kikundi cha Ujasiriamali cha ‘’Youth Empowerment” cha Mkokotoni kilichosaidiwa mtaji

kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao; Kikundi cha kilimo Mkombozi Fungurefu kilichosaidiwa mashine moja ya maji na mipira ya kusambazia maji na pembejeo za kilimo; pamoja na kuezeka jengo la jumuiya ya watu wasioona (ZANAB) liliopo Chaani Masingini. Vikundi 10 vinavyojishughulisha na masuala ya mabadiliko ya tabianchi vimepatiwa mafunzo kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi ambapo washiriki 40 walipata nafasi ya kushiriki katika mafunzo hayo. Aidha, msaada wa kifedha na vifaa vya ujenzi umetolewa katika shehia 11 zikiwemo Nungwi, Tazari na Kilindi zilizoathirika kwa upepo na mvua kubwa.

**BARAZA LA MJI KASKAZINI "B"**

**147.Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Baraza la Mji Kaskazini 'B' limeimarisha huduma za usafi wa mazingira, limefanya operesheni za usafi katika maeneo ya miji, masoko, utalii na uwekezaji ikiwemo Kiwengwa, Mahonda, Mangapwani na Kinduni na kufanikiwa kuzoa jumla ya tani 10,910 za taka. Wananchi kutoka shehia 31 wamehamasishwa juu ya usafi wa mazingira, uchimbaji karo na ujenzi wa vyoo ili kujikinga na maradhi yanayoweza kusababishwa na uchafu pamoja na kuweka ndoo 45 za kuhifadhia taka katika maeneo ya utalii ya Kiwengwa. Aidha, Baraza limefanya ukaguzi wa nyumba 2,015 na kubaini nyumba 15 kutokuwa na vyoo na nyumba 167 hazikuwa na karo za kuhifadhia maji machafu na kupewa muda wa kuchimba vyoo na karo, ambapo wote walirekebisha kasoro zao katika kipindi cha miezi mitatu.

**148.Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji miradi ya maendeleo Baraza la Mji Kaskazini 'B', limejenga ukumbi wa mitihani Skuli ya Sekondari Bumbwini Misufini na ujenzi wa barabara za kifusi za Donge kwa Kitarabu – Donge Fuasini (km 2) na Donge Mbiji – Donge Chechele (km 1) kwa lengo la kuimarisha huduma za usafirishaji na mawasiliano. Vile vile, Baraza limeezeka madarasa matatu, chumba cha maktaba pamoja na choo kimoja chenye matundu mawili katika skuli ya Kiwengwa na ujenzi wa vyoo vyenye matundu manane katika kituo cha dagaa Mangapwani.

**149.Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa ugatuzi kupitia sekta za elimu na afya, Baraza la Mji Kaskazini 'B' limehamasisha uandikishaji wa wanafunzi wa Msingi, Maandalizi na TUTU, ambapo jumla ya wanafunzi 4,679

(Wanawake 2387, Wanaume 2292) sawa na asilimia 98.92 ya makadirio wameandikishwa. Nauli za walimu 327 zimelipwa ili kuwawezesha kufika katika vituo vya kazi kwa wakati. Aidha, Baraza la Mji Kaskazini 'B' liliwahamasisha mama wajawazito kuhudhuria kliniki, kujifungulia vituoni na kuwapa elimu juu ya uzazi salama ambapo jumla ya mama 516 walijifungulia katika vituo vya Afya. Katika upatikanaji wa huduma za chanjo, watoto wapatao 15,739 wamepatiwa chanjo ya kusaidia makuzi yao.

150.**Mheshimiwa Spika,** huduma za ugani kwenye sekta za Kilimo, Uvuvi, Mifugo na Misitu zimeimarishwa. Baraza limewajengea uwezo wakulima 230 wa mboga katika Shehia 10. Mashamba darasa 10 ya Muhogo na 15 ya migomba yameanzishwa katika Shehia ya Kitope, Kinduni na Mbaleni ili kuongeza tija ya kilimo katika mazao hayo. Katika kupambana na uvuvi haramu Baraza lilifanya doria katika diko la Kiwengwa na kubaini utumiaji wa nyavu za macho madogo na nyavu za mishipi ambapo hatua za kisheria zilichukuliwa kwa wahusika. Kwa upande wa mifugo jumla wafugaji 794 wamepatiwa elimu ya kanuni bora za ufugaji na kubaini kichaa cha Mbwa. Kwa upande wa kuimarisha misitu na matunda jumla ya Miche 50,300 imeoteshwa katika vitalu vya Baraza ikiwemo mikarafuu 5,000, michungwa 1,000, mivinje 41,000, mitondoo 300, misaji 700, mizambarau 250 na miche mingine 2050.

151.**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mkoa wa Kaskazini Ungujauliidhinishiwajumla ya **Shilingi 15,365,100,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,397,700,000** ni mishahara, **Shilingi 631,700,000** matumizi mengineyona **Shilingi 13,335,700,000** ni ruzuku kwa Mabaraza ya Miji. Hadi kufikia Machi 2021, Mkoa umeshaingiziwajumla ya **Shilingi 7,888,667,175** sawa na asilimia **51**. Kati ya hizo **Shilingi 1,098,267,025** sawa na asilimia **79** ni mishahara, **Shilingi 102,503,972** sawa na asilimia **16** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 6,687,896,178** sawa na asilimia **50** ni ruzuku ya Mabaraza ya Miji. Mkoa umeidhinishiwa makusanyo ya **Shilingi 27,500,000** hadi kufikia Machi 2021 nakukusanya jumla **Shilingi 8,490,000** sawa na asilimia **31** ya makadirio. Vile vile, Barazala Mji Kaskazini "A" Unguja limeidhinishiwa makusanyo ya **Shilingi 1,000,900,000** na hadi kufikia Machi 2021, limekusanya jumla ya **Shilingi**

**808,598,622** sawa na asilimia 81. Kwa upande wa Baraza la Mji Kaskazini "B" limeidhinishiwa makusanyo ya **Shilingi 2,285,050,000** na hadi kufikia Machi 2021, Baraza limekusanya jumla ya **Shilingi 1,586,876,199** sawa na asilimia **69**.

**MKOA WA KUSINI PEMBA – FUNGU (D10)**

**PROGRAMU YA KUSIMAMIA SHUGHULI ZA SERIKALI KATIKA MKOA**

**152.Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mkoa wa Kusini Pemba ulipanga kusimamia shughuli za ulinzi na usalama, kuratibu ziara za viongozi wa kitaifa, kusimamia Mpango Mkakati wa Kitaifa wa kupiga vita udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto, kuendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya, wizi wa mazao na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za sekta na usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**153.Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia ulinzi na usalama jumla ya vikao 18 vya Kamati za ulinzi na usalama za Mkoa vilifanyika ambavyo vilijadili masuala kadhaa mfano udhibiti wa dawa za kulevya, mapambano dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia, udhibiti wa utoro wa wanafunzi shuleni na udhibiti wa biashara za magendo ya Karafuu. Kufuatia vikao hivyo, mikakati mbali mbali ya kupambana na matukio hayo iliandaliwa kwa mashirikiano makubwa baina ya vyombo vya ulinzi na usalama na jamii. Katika udhibiti wa magendo ya karafuu kwa mwaka 2020/2021 hakukua na tukio liliripotiwa ikilinganishwa na matukio mawili (2) ya magendo ya karafuu yaliyoripotiwa mwaka 2019/2020. Suala la dawa za kulevya na utoro wa wanafunzi limeongezeka ambapo matukio ya dawa za kulevya yalikua 58 kutoka 48 kipindi kilichopita, na utoro wa wanafunzi umeongezeka kufikia wanafunzi 85 kati ya 1000 kushindwa kuhudhuria Skuli kwa mwezi ukilinganisha na wanafunzi 75 kwa mwaka 2019/2020. Aidha, takwimu za Polisi zimeonesha kupungua kwa uhalifu kutoka matukio 217 mwaka 2019/2020 na kufikia 165 mwaka 2020/2021. Hivyo, juhudi mbali mbali za kupambana na masuala hayo zinaendelea kuchukuliwa ili kuhakikisha yanapungua.

**154.Mheshimiwa Spika,** Mkoa umeunda kamati ya kusimamia na kutatua migogoro ya ardhi kwa lengo la kuwa na mikakati shirikishi katika

kupunguza migogoro ya ardhi inayojitokeza kila uchao. Kamati hii imeundwa na wajumbe kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Chake Chake na Mkoani na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini ili ifuatilie kwa kina na kupata maamuzi ya pamoja ya usuluhishi wa migogoro ya ardhi. Kwa kipindi cha Julai - Machi 2020/2021, migogoro ya ardhi iliyoripotiwa katika Afisi za Wakuu wa Wilaya ni 30 (Mkoani 17, Chake 13). Takwimu hii inaonesha mafanikio ya kupungua kwa migogoro hiyo katika Mkoa ukilinganisha na mwaka 2019/2020 ambapo migogoro 48 iliripotiwa.

155.**Mheshimiwa Spika,** matukio 135 ya udhalilishaji yameripotiwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria ambapo matukio 86 yapo katika vituo vya Polisi kwa upelelezi, sita (6) yamesikilizwa na kumalizika Mahakamani na 34 yapo Mahakamani ukilinganisha na matukio 278 yaliyoripotiwa mwaka 2019/2020. Katika kupambana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia, elimu kwa wananchi kupitia Redio Jamii Mkoani na Istiqama Chake Chake imetolewa. Vile vile, Mkoa umetoa elimu ya kupambana na udhalilishaji kwa jamii katika Wilaya za Mkoani na Chake Chake kupitia ufadhili wa Shirika la Kimataifa la kuhudumia Watoto Ulimwenguni (UNICEF) katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji.

156.**Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Mkoa umefuatilia maendeleo ya Ujenzi wa barabara (4) nne zilizojengwa na zinazoendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hizo ni Ole – Kengeja kilomita 35 na Gombani – Pagali kilomita 1.8 ambazo tayari zimekamilika. Aidha, barabara ya Kipapo – Mgelema - Wambaa yenye urefu wa kilomita tisa (9) na Kijangwani - Birikau yenye urefu wa kilomita 4.2 zinaendelea kujengwa kupitia ufadhili wa Taasisi ya *Ifraji Zanzibar Foundation*. Hata hivyo, Mkoa, unaendelea kusimamia ukarabati wa jengo la Hospitali ya Chake Chake, ZRB Gombani, ujenzi wa Kalavati Mkanyageni. Vile vile, Mkoa unaendelea kufuatilia kwa karibu sana ujenzi wa Bwawa la mradi wa kilimo cha umwagiliaji bonde la Mlemele - Shehia ya Dodo Pujini. Aidha, mradi wa kilimo cha umwagiliaji bonde la Dodeani tayari umekamilika.

**157.Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia sekta ya elimu, Mkoa umefanya ziara za ufuatiliaji kwa Skuli 70 za Maandalizi na Msingi za Wilaya ya Chake Chake na Mkoani kwa lengo la kuangalia utendaji pamoja na changamoto zinazoikumba sekta ya elimu. Changamoto mbali mbali zilibainika ikiwa ni pamoja na upungufu wa walimu wa masomo ya Sayansi kwa baadhi ya Skuli na utoro wa walimu na wanafunzi. Aidha, suala la uhaba wa madarasa na vikalio (madawati) limebainika kwa baadhi ya skuli. Hata hivyo taratibu za kuzitatua changamoto hizo zimeanza kuchukuliwa kwa mashirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wadau wengine wa maedeleo.

**PROGRAMU YA UENDESHAJI NA UTAWALA**

**158.Mheshimiwa Spika,** Mkoa umeweka mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia vitendea kazi Wafanyakazi, kufanya matengenezo madogo madogo ya Ofisi, kulipa stahiki za watumishi ikiwemo posho la likizo kwa watumishi 25, mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi watatu (3) na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wawili (2). Mkoa unaendelea na ujenzi wa nyumba ya makaazi ya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa katika eneo la Pagali ambayo imefikia hatua ya kufunga ukanda. Vile vile, jumla ya wananchi 580 (wanaume 265 na wanawake 315) wanaoshi katika mazingira magumu wamepatiwa msaada wa Shilingi 5,000 kwa kila mmoja zinazotolewa kila mwezi, ambapo jumla ya **Shilingi 11,600,000** zimetolewa.

**PROGRAMU YA USIMAMIZI WA SERIKALI ZA MITAA**

**BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE**

**159.Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza limepanga kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kuimarisha usafi wa mazingira na kutekeleza miradi mbali mbali ya wananchi ikiwemo kuimarisha huduma za Afya ya Msingi, Elimu ya Maandalizi na Msingi na huduma za Ugani.

**160.Mheshimiwa Spika** Katika kulinda na kutunza afya za wananchi, Baraza limefanikiwa kuzoa taka ngumu tani 6,900 na kuzipeleka katika jaa kuu la Vitongoji. Sambamba na hilo, Baraza lilifanikiwa kusafisha misingi ya maji ya taka yenye urefu wa mita 4,250. Baraza limevipatia vituo 16 vya afya vifaa tiba na vitendanishi, Elimu ya Afya kwa Shehia 32 za Wilaya ya Chake Chake, huduma za kinga natiba kwa jamii, huduma ya chanjo kwa watoto

wa kike 193 walio chini ya umri wa miaka 14 na chanjo kwa mama wajawazito 1,871. Aidha, Baraza limefanikiwa kusambazachanjo katika vituo 16 vya afya ili kutokomeza maradhi ya miripuko, maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

161.**Mheshimiwa Spika,** Katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo ya wananchi inayotekelezwa kupitia mapato ya ndani Baraza la Mji Chake Chake limesaidia kupunguza tatizo la uhaba wa madarasa katika Skuli ya Maandalizi Machomane kwa kumalizia ujenzi wa madarasa mawili (2) ya kusomea, kumalizia ujenzi wa Ofisi mbili (2) za Walimu katika Skuli ya Msingi Kwale ambayo imegharimu jumla ya Shilingi 44,166,252. Baraza katika kuimarisha huduma za afya limefanya matengenezo ya vituo vitatu vya afya ambavyo ni Shungi, Tundauwa na Vikunguni kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma za afya katika maeneo hayo.

162.**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya elimu ya Maandalizi na Msingi, jumla ya wanafunzi 9,505 wameandikishwa. Kati ya hao wanafunzi 4,451 ni wa skuli za Maandalizi (wanaume 2,247 na wanawake 2,204) na wanafunzi 5,054 wa skuli za msingi (wanaume 2,533 na wanawake 2,521) kwa mwaka 2020/2021 ukilinganisha na wanafunzi 9,175 walioandikishwa mwaka 2019. Kwa upande wa huduma ya lishe, Baraza limewapatia uji Wanafunzi 4,073 wa Maandalizi na kulipa posho kwa walimu 44 wa vituo 22 vya TUTU.

163.**Mheshimiwa Spika,** Baraza limeendelea kuimarisha huduma za ugani kwakutoa mafunzo ya namna bora ya kutayarisha, kupanda na kulea miche ya migomba na muhogo kupitia shamba darasa, ambapo jumla ya wakulima 4,768 wamefaidika na mafunzo hayo. Wananchi 54 wamepatiwa mafunzo ya uhifadhi wa misitu ya jamii, wananchi 59 wameilimishwa juu ya uimarishaji wa vitalu na wananchi 118 wamepewa mafunzo ya ukulima bora wa mwani. Aidha, mafunzo ya ufugaji yametolewa kwa wananchi 460 juu ya ufugaji wa Ng'ombe, wananchi kwa 346 ufugaji Mbuzi, wananchi 274 kwa ufugaji wa Kuku, wananchi 58 kwa ufugaji wa Samaki, na wananchi 49 kwa ufugaji wa Majongoo. Pamoja na hayo, Baraza limesaidia vifaa vya kilimo kwa kikundi cha *Mgelema Youth Cooperation* kilichopo Shehia ya Mgelema.

**164.Mheshimiwa Spika** Katika kuwawekea mazingira bora ya kazi watumishi na Madiwani, Baraza limetoa huduma za kawaida kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa Umeme, matengenezo ya vyombo vya usafiri, huduma za mawasilisno. Aidha, Baraza limetoa usafiri kwa watumishi ili kushajihisha kiwango cha uwajibikaji. Aidha Malipo ya mishahara kwa waajiriwa 1,165, vibarua wa muda watano (5) na Waheshimiwa Madiwani 19 yamelipwa.

**BARAZA LA MJI MKOANI**

**165.Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Mji Mkoani, limepanga kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kuimarisha usafi wa mazingira na kutekeleza miradi mbali mbali ya wananchi ikiwemo kuimarisha huduma za Afya ya Msingi, Elimu ya Maandalizi na Msingi, huduma za Ugani na kutoa huduma za kijamii.

**166.Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha usafi wa mazingira Baraza limefanikiwa kufanya usafi wa Mji kwa kuzoa jumla ya tani za taka ngumu 1,100 na kuzitupa katika jaa kuu la Chokaani. Baraza limefanya usafi wa msingi mitatu (3) ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 1.2. Baraza limetoa elimu ya usafi wa mazingira kwa wakaazi wa Mji wa Mkoani ambapo Kamati kumi (10) zimeundwa zinazojumuisha Shehia za Uweleni, Makombeni na Ng'ombeni. Baraza limesambaza jumla ya madastibini 45 katika maeneo mbali mbali ya Mji wa Mkoani ili kudhibiti utupaji wa taka kiholela.Aidha, katika kusimamia ukusanyaji wa mapato, ziara za kuimarisha ukusanyaji wa mapato zimefanyika katika Shehia 36 za Wilaya ya Mkoani, pamoja na kufanya mikutano ya kushajihisha wananchi juu ya ulipaji wa kodi kwa hiari na kwa wakati.

**167.Mheshimiwa Spika,** katika kutoa huduma za uendeshaji, Baraza limenunua vitendea kazi kwa ajili ya Ofisi, vifaa vya kuandikia, matengenezo ya vyombo vya usafiri zikiwemo gari tatu (3) na vespa tano (5) pamoja na kuwapatia Waheshimiwa Madiwani na watendaji stahiki zao. Aidha, Baraza limewapatia mafunzo ya muda mrefu mtumishi mmoja (1) na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi (12) na limewapatia Waheshimiwa Madiwani 18 mafunzo ya muda mfupi. Katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya

maendeleo ya wananchi kupitia Wadi, Baraza limesaidia kupunguza tatizo la madarasa katika Skuli ya Maandalizi Tumbi na Wambaa. Aidha, Baraza katika kuimarisha utoaji wa huduma za elimu limefanya ukarabati wa Skuli ya Ng'ombeni na ujenzi wa Kalvati ya Mtemani –Bogoa umefanyika kwa lengo la kurahisha upatikanaji wa huduma.

**168.Mheshimiwa Spika,** Katika kusimamia sekta ya elimu, Baraza limefanikiwa kuandikisha jumla ya wanafunzi 8,197 Kati ya hao wanafunzi 3,689 ni wa Maandalizi (wanawake 1,914 na wanaume 1,775) na wanafunzi 4,511 wa Msingi (wanaume 2,362 na wanawake 2,149) wameandikishwa kwa mwaka 2020/2021,kutokawanafunzi 9,171 walioandikishwa kwa mwaka 2019/2020. Sambamba na kuandikisha jumla ya wanafunzi wa TUTU 1,518 wakiwemo (wanaume 783 na wanawake 795). Aidha, jumla ya wanafunzi 2,547 wa Maandalizi wamewapatia huduma ya lishe na Walimu 138 wa vituo vya TUTU wamepatiwa posho maalum. Vile vile, jumla ya katuni 1,922 za mabuku, chaki na manila zimegaiwa kwa skuli 36 za Wilaya ya Mkoani.

**169.Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa sekta ya Afya, jumla ya vituo vya afya 18 vimepatiwa vifaa tiba na visivyokuwa tiba. Aidha, Baraza limetoa huduma za tiba na kinga kwa jamii ambapo Chanjo mbalimbali zimetolewa kwa akina mama 1,724 na watoto 26,064. Jumla ya mama wajawazito 2,510 wamehudhuria kliniki kabla ya kujifungua, na mama 386 baada ya kujifungua. Hata hivyo Baraza limefanikiwa kutoa huduma za mkoba katika Shehia zote 36 za Wilaya ya Mkoani ambapo jumla ya huduma za mkoba 207 zimetolewa, sambamba na kutoa elimu ya afya kwa wafanyakazi wa vituoni.

**170.Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa huduma za ugani, Baraza limetoa elimu kwa Wakulima 561 juu ya matumizi bora ya mbolea, uvunaji na uhifadhi wa mazao, utumiaji bora wa viatilifu na uzalishaji wa mazao mbali mbali, na kutoa elimu juu ya ufugaji wa kisasa kwa wafugaji 56. Baraza kwa kushirikiana na Wizara ya kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo lilisimamia utekelezaji wa miradi mbali mbali katika Shehia ya Dodo Pujini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bwawa la umwagiliaji bonde la Mlemele. Aidha, Baraza lilisimamia ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 2.3 kwa kiwango cha fusi kutoka Dodo hadi Mlemele.

**171. Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanikiwa kutoa elimu ya ugani kwa Wafugaji 56 katika Shehia ya Chokocho, Kisiwapanza na Kukuu Kangani. Jumla ya wanyama 1,892 walipatiwa chanjo ya kuwakinga na maradhi mbali mbali wakiwemo Ng'ombe 1,004, Mbuzi 180, Kuku 180, Paka 154, Punda 14, na Mbwa 360. Aidha, jumla ya shamba darasa nne (4) zimeanzishwa kwa wakulima wa kilimo cha mpunga katika Shehia ya Mgagadu - bonde la Kimbuni, kilimo cha migomba Shehia ya Mgagadu, kilimo cha mboga mboga Shehia ya Wambaaa na Kiwani.

**172. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mkoa wa Kusini Pemba uliidhinishiwa **Shilingi 14,682,500,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,124,200,000** ni mishahara, **Shilingi 994,690,000** matumizi mengineyo na **Shilingi 12,563,610,0**00 ni ruzuku ya Baraza la Mji Chake na Baraza la Mji Mkoani. Hadi kufikia Machi 2021, Mkoa umeingiziwa **Shilingi 7,286,083,750** sawa na asilimia **50**. Kati ya fedha hizo **Shillingi 972,767,415** sawa na asilimia **87** ni misharahara, **Shilingi 172,361,725** sawa na asilimia **17** ni matumizi mengineyo, na **Shilingi 6,140,954,610** sawa na asilimia **49** ni ruzuku. Aidha, Mkoa uliidhinishiwa kuchangia **Shilingi 25,700,000** katika Mfuko Mkuu wa Hazina na kuchangia **Shilingi 12,115,000** sawa na asilimia 47 ya makadirio. Baraza la Mji Chake liliidhinishiwa makusanyo ya mapato ya ndani **Shilingi 600,549,400** na kukusanya **Shilingi 519,720,000** sawa na asilimia **87**. Vile vile, Baraza la Mji Mkoani liidhinishiwa makusanyo ya mapato ya ndani **Shilingi 374,720,000** na kukusanya **Shilingi 302,540,736** sawa na asilimia **81**.

**MKOA WA KASKAZINI PEMBA - FUNGU D11**

**PROGRAMU YA KUSIMAMIA SHUGHULI ZA SERIKALI KATIKA MKOA**

173.**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mkoa wa Kaskazini Pemba ulipanga kudumisha amani, usalama, utulivu na mshikamano kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na wananchi wenyewe; kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa, ulipaji wa stahiki za watumishi, Ukarabati wa majengo ya Ofisi za Mkoa na Wilaya; kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi; kuratibu sherehe na ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa; kufuatilia, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya sekta katika Mkoa; na kuendeleza mapambano ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

174.**Mheshimiwa Spika,** katika kudumisha amani, usalama, utulivu na mshikamano uliopo, vikao 39 vya Kamati za Usalama za Mkoa na Wilaya vilifanyika vilivyolenga kujadili na kuweka mikakati ya kupambana na viashiria vya uvunjifu wa amani. Matokeo yaliyopatikana katika vikao hivyo ni kufanikisha kufanyika kwa amani na usalama kwa Uchaguzi mkuu wa Zanzibzr na uchaguzi mdogo wa Mwakilishi wa Jimbo la Pandani, kupungua kwa matukio ya uhalifu na uvunjifu wa amani pamoja na kuchukuliwa hatua za kisheria wahalifu waliobainika. Matokeo mengine ni pamoja na wananchi kukubaliana na agizo la Serikali kuacha uchimbaji wa mawe katika maeneo yaliyopigwa marufuku katika Wilaya ya Micheweni.

175.**Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Kaskazini Pemba ulibahatika kutembelewa na viongozi wakuu watano wa Kitaifa ambao ni Rais wa Zanzibar Dkt Hussein Ali Mwinyi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Rais Mstaafu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein, na aliyekuwa Makamo wa Kwanza wa Rais Hayati Mheshimiwa Seif Shariff Hamad. Ziara hizo zimeleta mchango mkubwa katika maendeleo ya Mkoa kutokana namaelekezo, maagizo na ahadi zilizotolewa na viongozi hao ambapo utekelezaji wake unaendelea kuratibiwa kupitia Wizara za Kisekta. Aidha, zimewezesha wananchi kuendeleza

maridhiano na kutoa mashirikiano kwa viongozi wa ngazi mbali mbali na kupelekea kufanya shughuli zao za kijamii na kiuchumi kwa amani na utulivu bila mvutano wowote na itikadi za kisiasa.

176.**Mheshimiwa Spika,** katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa watoto na unyanyasaji wa Kijinsia, vikao 14 na mikutano 15 imefanyika katika Shehia mbali mbali za Mkoa kwa kushirikiana na wadau mbali mbali kwa lengo la kutathmini ukubwa wa tatizo na kupanga mikakati ya kukabiliana na kupunguza kasi ya udhalilishaji. Miongoni mwa mikakati hio ni kuelimisha jamii kuondokana na muhali na kuepuka kusuluhisha kesi za udhalilishaji katika ngazi za familia, na kufuatilia kwa karibu nyenendo za watoto ili kugundua kama kuna mabadiliko. Takwimu zimeonyesha matukio ya udhalilishaji yameanza kupungua ambapo jumla ya matukio 138 yameripotiwa kwa kipindi cha Julai – Machi 2020/2021 ukilinganisha na matukio 153 katika kipindi kilichopita, hatua zilizochukuliwa dhidi ya matukio hayo ni kwamba matukio 38 yamefikishwa mahakamani, 15 yametolewa hukumu na 85 yanaendelea na upelelezi.

177.**Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia utekelezaji wa malengo ya Sekta nyengine katika Mkoa, miradi 22 ya maendeleo imekaguliwa miongoni wa miradi hiyo ni ujenzi wa Afisi ya Chuo cha Mafunzo Wete, ujenzi wa nyumba za Askari wa KMKM Kiuyu Mbuyuni, Ujenzi wa Soko la samaki na matunda Micheweni, na mradi wa nyumba za Maafa Tumbe. Lengo la Ukaguzi huo ni kuona ubora wa miradi na thamani ya fedha iliyotumika na muda uliopangwa kuanza na kumalizika kwa mradi pamoja na changamoto nyengine zilizojitokeza. Matokeo ya ukaguzi ni kuwa baadhi ya miradi ilionekana haiko sawa na kutolewa maelekezo ya kuifanyia marekebisho.Shughuli nyengine zilizotekelezwa na Mkoa ni pamoja na kushirikiana naWizara ya Afya kupitia kitengo cha kupambana na maradhi yasiyoambukiza kufanikisha zoezi la upimaji wa Saratani ya Matiti na Shingo ya kizazi katika Hospitali ya Wete.Aidha, Mkoa umeweza kusimamia na kushajihisha zoezi la uchangiaji wa damu salama kwa njia ya Bonanza katika kiwanja cha Jamhuri hall na jumla ya chupa 178 za damu salama zilipatikana.

**178. Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia huduma za utawala na uendeshaji za Mkoa, Wilaya na Shehia zake, Mkoa umeendelea kufanya matengenezo ya majengo ya ofisi na nyumba za viongozi. Mkoa umeendelea kuimarisha mazingira bora ya Watumishi kwa kuwalipa stahiki zao, ikiwemo malipo Baada ya saa za kazi 14, likizo 13, safari za kikazi 12, Mishahara na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF). Aidha, Afisi imesimamia ukarabati mdogo wa nyumba ya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, upatikanaji wa vifaa, zikiwemo Kompyuta tano (5) na vifaa vya usafi. Afisi imefanya matengenezo ya gari, vespa na pikipiki na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi wanne (4) katika fani na ngazi mbali mbali. Matokeo ya hatua hizo ni kuimarika kwa uwajibikaji wa watumishi na kuwapatia wananchi huduma bora na kwa wakati ikiwemo vyeti vya kuzaliwa.

**179. Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia maendeleo ya elimu, Mkoa na Wilaya zake umefanya vikao vinane (8) na walimu wakuu kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji ikiwa ni pamoja na kuchukuwa juhudi na kuweka mikakati ya kuongeza kiwango cha Ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya Taifa. Miongoni mwa mikakati iliyowekwa ni kupandisha kiwango cha ufaulu na madaraja ya juu kutoka asilimia 56 ya mwaka 2020 kufikia asilimia 80 kwa mwaka 2021. Kadhalika Kupunguza kiwango cha kufeli kutoka asilimia 43 hadi asilimia 10 kwa mwaka 2021. Aidha, Mkoa umesimamia uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza 10,773 (wasichana 5,158 na wavulana 5,615). Maandalizi waliandikishwa wanafunzi 7,127 (wavulana 3,483 na wasichana 3,644). Wanafunzi wa TUTU walioandikishwa ni 2,772.

**PROGRAMU YA UTAWALA NA UENDESHAJI**

**180. Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia masuala ya wananchi, Mkoa umejiwekea utaratibu maalum wa kusikiliza kero za wananchi kila siku ya Alhamisi. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya malalamiko 136 yalipokelewa na kusikilizwa. Malalamiko yaliyopokelewa yalihusiana na migogoro ya ardhi, vitendo vyaudhalilishaji, madai ya fidia, uhalifu wa fedha, tatizo la ukosefu wa Maji safi na salama, upatikanaji wa umeme, matengenezo ya barabara za ndani na migogoro ya kifamilia. Baadhi ya malalamiko hayo yamepatiwa ufumbuzi katika ngazi ya Mkoa na Shehia, na yale yaliyo nje ya uwezo wa Mkoa yameratibiwa kwa kufikishwa kwenye mamlaka husika.Vile

vile, huduma za utumishi na uendeshaji ikiwemo mafunzo kwa watumishi, ununuzi wa vitendea kazi pamoja na malipo ya stahiki kwa watumishi zimetolewa.

**PROGRAMU YA USIMAMIZI WA SERIKALI ZA MITAA**

**BARAZA LA MJI WETE**

181.**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza la Mji Wete lilipanga kutekeleza miradi ya kijamii na kiuchumi ikiwemo ukarabati wa skuli, ukarabati wa ukumbi wa mkutano wa Jamhuri Hall, Ukarabati wa masoko, diko na ujenzi wa Bustani ndani ya Mji, kufanya usafi wa mji na kuimarisha shughuli za ukusanyaji wa mapato. Katika uendeshaji wa shughuli zake.

182.**Mheshimiwa Spika,** Baraza la Mji Wete limeendelea kufanya usafi wa mazingira katika maeneo yote ya Mji ambapo jumla ya tani 9,954 za taka ngumu zimezolewa, misingi ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 8 imesafishwa na kuondosha majaa sita yasiyo rasmi ndani ya Mji wa Wete. Baraza linaendelea na upandaji wa bustani katikati ya barabara kuanzia Ikulu ya Wete hadi mtaa wa Limbani pamoja na kuhuwisha Bustani ya Jamhuri. Baraza limefanya ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo vifaa vya usafi, shajara na kufanya matengenezo ya vyombo vya usafiri, vikao vitatu vya Baraza la Madiwani na sita vya kamati za kudumu za madiwani vimefanyika pamoja na kulipa stahiki za Wafanyakazi na Madiwani kwa wakati. Aidha, Baraza limefanya ukarabati wa soko la matunda Wete na diko liliopo Bandarini Wete.

183.**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kuendeleza elimu ya msingi na maandalizi, Baraza limetoa posho la nauli kwa walimu 163, posho za wasaidizi 23 wa vituo vya TUTU na posho baada ya saa za kazi kwa watumishi 14. Barza limeendesha zoezi la uhamasishaji wa uandikishaji wa wanafunzi wapya kwa mwaka 2021 ambapo jumla ya wanafunzi 8,980 (wanaume 4,596 na wanawake 4,384) wameandikishwa ikijumuisha Maandalizi 3,200 (wanaume 1,629 na wanawake 1,571) na Msingi ni 5,780 (wanaume 2,967 na wanawake 2,813). Vile vile mikutano ya Kamati za maendeleo ya Skuli imefanyika ambapo wazazi wamenasihiwa na

kusisitizwa kufuatilia maendeleo ya watoto maskulini kwani kumeibuka tatizo la baadhi ya wanafunzi kutoroka madarasani.

184. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Idara ya huduma za kinga na afya ya Msingi, Baraza limeweza kuvipatia vituo vya afya 21 vifaa tiba na vitendanishi kwa utoaji wa huduma bora za afya, ambavyo ni; mashine ya kupimia wingi wa damu, vifaa vya usafi na usambazaji wa chanjo vituoni. Baraza limesaidia upatikanaji wa huduma za chanjo kwa mama wajawazito 11,333, Chanjo ya matone ya polio kwa watoto 12,575, Chanjo ya kuzuia maradhi ya kuharisha kwa watoto 4,925, Chanjo ya surua ya kwanza wamepatiwa watoto 5,619 na Chanjo ya BCG watoto 5,837. Chanjo hizi zimepelekea ukuwaji mzuri wa watoto na kuwakinga dhidi ya maradhi mbalimbali. Kadhalika, Baraza la Mji Wete limewezesha kufanyika kwa ukarabati wa kituo cha ''RCH" kilichopo katika majengo ya Hospitali ya Wete. Aidha, Elimu ya maambukizo ya virusi vya UKIMWI imetolewa na wananchi 224 (wanaume 105 na wanawake 119) wamefika vituoni kupata huduma za upimaji virusi vya UKIMWI kwa hiyari na vipimo vyote vilionyesha kuwa hakuna aliyeambukizwa.

185. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani, Baraza limeendelea kusimamia kitalu cha miche kilichopo Chamanangwe ambacho kimeotesha miche ya minazi 750, Miparachichi 400, michugwa 1,200, midimu 1,200, mipapindi 400, mishokishoki 300, mifenesi 100, mipapai 600, mibirimbi 300, michenza 300, na mistafeli 300. Elimu kwa wakulima imeendelea kutolewa ambapo wakulima 9,687 na wafugaji 863 wamefikiwa wakiwemo wakulima wa mwani 550. Jumla ya mifugo 669 imetibiwa wakiwemo ng'ombe 223, mbuzi 51, mbwa saba (7), paka 10, kuku 351, njiwa 25 na punda wawili (2). Vile vile Kamati za uvuvi zimeilimishwa juu ya hifadhi ya matumbawe katika shughuli zao za uvuvi kwa lengo la kutunza mazingira na kuzuia uvuvi haramu.

186. **Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kusaidia vijana, wazee na watu wenye ulemavu, Baraza limesaidia mashine tatu (3) za umwagiliaji maji kwa vikundi vya; *Umoja ni nguvu* – Limbani Mikindani, *Subira Njema* – Mtemani na *Mwanzo Mgumu*-Mashuga Kisiwani. Pia Baraza liimesaidia vifaa vya ushoni kwa ajili ya kitengo cha ushonaji cha Baraza la Vijana la Wilaya ya

Wete, msaada huo umetolewa kwa lengo la kuyawezesha makundi hayo kuendelea na harakati zao za kujipatia kipato cha halali kupitia kilimo na ufundi wa ushonaji nguo.

**HALMASHAURI WILAYA YA MICHEWENI**

**187. Mheshimiwa Spika,** Halmashauri imeendelea kufanya usafi na kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa usafi wa mazingira katika shehia zote za Wilaya ya Micheweni, Aidha imeendelea kufanya matengenezo ya Ofisi, ununuzi wa vitendea kazi, kufanya matengenezo ya vyombo vya usafiri na kulipa stahiki za watumishi na Waheshimiwa Madiwani. na kufanya vikao vya kiutendaji vya Baraza la Madiwani, Wadi na Kamati za Mashauriano za Shehia.

**188. Mheshimiwa Spika,** Huduma ya afya ya mama na mtoto imeimarika, kwa kuongezeka wateja wapya 309, Wakunga wa jadi 51 wamepatiwa mafunzo kuhusu namna ya kuwahamasisha mama wajawazito kujifungua katika vituo vya Afya na umuhimu wa chanjo kwa watoto wakike waliofikia umri wa miaka 14. Utoaji wa chanjo za watoto chini ya miaka mitano (5) umefanyika kwa asilimia 83 ukilinganisha na asilimia 81.6 mwaka 2019/2020. Katika mapambano dhidi ya malaria, Halmashauri kwa kushirikiana na kitengo cha kumaliza malaria imefanikiwa kunyunyizia viatilifu katika kaya 3,658 kwa shehia sita (6) za Wilaya ya Micheweni. Aidha, Halmashauri imeweza kusimamia vituo vya Afya 14 ambavyo 11 ni daraja la kwanza na vitatu (3) ni daraja la pili.

**189. Mheshimiwa Spika,** idadi ya ufaulu wa wanafunzi wa michepuo na vipawa maalum umeongezeka ambapo, kwa mwaka 2018/2019 ni 84, mwaka 2019/2020 ni 102 na mwaka 2020/2021 ni 168. Halmashauri imezipatia skuli 28 za msingi na maandalizi huduma ya maji, umeme, kufanyiwa matengenezo madogo madogo na kusambaza vifaa vya kusomea kwa wanafunzi, ikiwemo usambazaji wa mabuku na chaki vikiwemo vituo 91 vya TUTU. Pia, uhamasishaji wa uandikishaji wa wanafunzi wapya umefanyika ambapo jumla ya wanafunzi 8,920 wameandikishwa kati ya hao 4,993(wanawake 2,518 na wanaume 2,475) darasa la kwanza, 1,605(wanawake 865 na wanaume 740) maandalizi na 2,322 TUTU.

190. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo, imefanya matayarisho ya kilimo cha mpunga msimu wa uzalishaji 2020/2021 ikiwa malengo ya ukulima ni ekari 4,400, kati ya hizo, jembe la mkono ni ekari 3,300 na trekta ni ekari 1,100. Ekari 4,017.25 zimeshachimbuliwa kwa jembe la mkono, ekari 240 kwa trekta na ekari 3,952.25 zimeshasiwa/kupandwa. Matarajio ya mavuno kwa msimu huu ni tani 6,487.88 katika eneo lenye ukubwa wa ekari 4,325.25 sawa na tani 1.5 kwa ekari moja.

191. **MheshimiwaSpika,** kwa mwaka fedha 2020/2021 Mkoa wa Kaskazini Pemba uliidhinishiwa **Shilingi 13,408,940,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,226,400,000** ni mishahara, **Shilingi 1,078,340,000** matumizi mengineyo na **Shilingi 11,104,200,000** ruzuku ya Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya Micheweni. Hadi kufikia Machi 2021, Mkoa umeingiziwa jumla **Shilingi, 8,154,356,219** sawa na asilimia **61**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 961,550,495** sawa na asilimia **78** ni mishahara, **Shilingi 152,342,000** sawa na asilimia **14** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 7,040,463,724** sawa na asilimia **63** ni ruzuku ya Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya Micheweni. Mkoa uliidhinishiwa kuchangia **Shilingi 25,476,000** katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Hadi kufikia Machi 2021, Mkoa umekusanya **Shilingi 9,220,000** sawa na asilimia 36. Aidha, Bazara la Mji Wete lilipanga kukusanya mapato ya **Shilingi 375,500,265** na kukusanya **Shilingi 363,145,400** sawa na asilimia **97** ya makadirio. Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni iliidhinishiwa kukusanya **Shilingi 300,000,000** na kukusanya **Shilingi 281,879,293** sawa na asilimia **94**.

**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII – FUNGU D12**

**192. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2021, Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii umefanikiwa kuzalisha jumla ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi 11,436 kwamaombi ya awali (Wanawake 4,835na Wanaume 6,601) sambamba na uzalishaji wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi 4,953(wanaume 2,476nawanawake 2,477) kwa waombaji wa maombi ya pili. Kwa upande wa Usajili wa Vizazi hai Wakala umefanikiwa kusajili jumla ya Vizazi hai 114,273(wanawake 57,946nawanaume ni 56,327). Na vifo vilivyosajiliwa ni 1,755, (wanawake ni 688na wanaume 1,067) na kusajili ndoa 252na Talaka 25. ***Angalia Kiambatisho namba 12***

**193. Mheshimiwa Spika**, Wakala kupitia Kampuni ya *Z-IT Solutions* ya Zanzibar imefanikiwa kukamilisha Mfumo wa Usajili wa Wakaazi wasiokuwa Wazanzibari kwa lengo la kuwapatia Vitambulisho, ambapo unategemewa kuanza kutumika rasmi kwa mwaka wa fedha 2021/22. Aidha Wakala imefanikiwa kuendeleza Mfumo wa CRVS katika Hospitali 12 (Bububu - Jeshini, KMKM, Alrahma, Global na Tawakal, Hospitali ya Mnazi mmoja, Mwembeladu, Fuoni, Makunduchi, Kivunge kwa Unguja na Hospitali ya Wete kwa Pemba).

**194. Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu ya Utumishi na Uendeshaji, Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii imewapatia mafunzo ya muda mrefu Wafanyakazi tisa (9) (Shahada ya pili ununuzi na ugavi mmoja (1), Shahada ya kwanza ya Uhifadhi wa Kumbukumbu mmoja (1), shahada ya kwanza katika fani ya Rasilimali watu watatu (3) Stashahada katika fani ya Tehama wawili (2). Aidha mafunzo maalum ya muda mfupi kwa wafanyakazi wawili (2) yametolewa kwa lengo la kuwajengea uwezo na ufanisi katika utendeji kazi.

**195. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,909,600,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,475,000,000** ni mishahara, **Shilingi 2,434,600,000** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 1,000,000,000** kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi

2021, Ofisi imeingiziwa **Shilingi 1,697,890,922** sawa na asilimia **35**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,147,341,922** sawa na asilimia **78** ni mishahara, **Shilingi 550,549,000** sawa na asilimia **23** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 127,000,000** sawa na asilimia **13** kwa kazi za maendeleo. Kwa upande wa mapato Ofisi iliidhinishiwa kukusanya **Shilingi 626,512,000** na kukusanya **Shilingi 434,553,460** sawa na asilimia **69** ya makadirio ya mwaka.

## MWELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**196. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo;

i. Kuimarisha ulinzi na usalama pamoja na kuondosha wizi wa mifugo na mazao kwa lengo la kudumisha amani, utulivu, umoja na maendeleo ya Zanzibar;
ii. Kuimarisha usafi wa miji kwa ajili ya kulinda afya za wananchi na kuvutia wageni wanaokuja Zanzibar;
iii. Kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato katika Serikali za Mitaa na kutumia mapato hayo kutoa huduma bora kwa wananchi
iv. Kuwajengea wajasiriamali masoko ya kudumu ya kufanyia biashara, kuwawekea utaratibu wa kulipa tozo mara moja kwa mwaka na kuwapatia vitambulisho;
v. Kuendeleza mapambano ya vitendo vya udhalilishaji wa watoto na unyanyasaji wa kijinsia katika ngazi ya Shehia, Wilaya na Mikoa;
vi. Kuimarisha usuluhishi wa migogoro ya ardhi katika jamii na kusimamia matumizi sahihi ya ardhi ya Zanzibar;
vii. Kuimarisha mifumo ya usajili wa matukio ya kijamii ili kuwarahisishia wananchi na wageni kupata huduma kwa wakati;
viii. Kuimarisha usajili na uratibu wa Jumuiya zisizo za Kiserikali ili zitoe mchango katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

ix. Kuendeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya Afisi, mahanga na nyumba za Maafisa wa Idara Maalum za SMZ;
x. Kuimarisha mazingira ya kambi za Idara Maalum za SMZ Mijini na Vijijini;
xi. Kuendelea kuwajengea uwezo Maofisa na Wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ kwa kuwapatia vifaa na mafunzo ya kisasa;
xii. Kuimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula kupitia Idara Maalum za SMZ.
xiii. Kuendeleza mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa, kutokuwajibika, uzembe, ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha na mali za Serikali.

**197. Mheshimiwa Spika,** baada ya kuonesha vipaumbele, naomba kuwasilisha mwelekeo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa kila fungu.

**198. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inatekeleza majukumu yake kupitia programu kubwa 18. Programu hizo zimegawanyika katika mafungu D01 hadi D12. Fungu D01 ni Programu zinazotekelezwa na Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu, Mafungu D02 hadi D06 yanahusu Idara Maalum za SMZ, Mafungu D07 hadi D11 ni Programu za Mikoa na Fungu D12 ni Programu za Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii.

**PROGRAMU ZA MAKAO MAKUU FUNGU-D01**

**199. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Idara za Makao Makuu imepanga kutekeleza yafuatayo;

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA OR - TMSMIM-SMZ**

**PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA ORTMSMIM**

**200. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji imepanga kuimarisha usimamizi wa masuala ya kiutumishi ikiwemo kuwajengea uwezo watumishi; kufanya ukaguzi wa kila

robo mwaka unaohusiana na rasilimali fedha na rasilimali watu; na kuwapatia vitendea kazi na stahiki watumishi.

201. **Mheshimiwa Spika,** iIi Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 4,070,713,101**. Kati ya hizo **Shilingi 2,418,440,506** kwa matumizi mengineyo, **Shilingi 998,972,595** kwa mishahara na stahiki na **Shilingi 653,300,000** kwa ruzuku ya Wakala wa Ulinzi JKU na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ.

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA KAZI ZA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

202. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2021/2022, Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kuandaa bajeti na mpango kazi wake; kuandaa maandiko ya miradi ya Maendeleo ya Wizara pamoja na kuandaa Sera mpya ya Serikali za Mitaa; kufanya utafiti wa usimamizi wa usafi wa Miji na utafiti wa kuibua vyanzo na uvujaji wa mapato ya Serikali za Mitaa; kufanya ufuatiliaji na tathmini wa program na miradi inayotekelezwa na Afisi na kuandaa muongozo wa fedha za Serikali za Mitaa wanazopatiwa wajasiriamali vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

203. **Mheshimiwa Spika,** iIi Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 623,732,950**. Kati ya hizo **Shilingi 461,044,000** kwa matumizi mengineyo, na **Shilingi 162,688,950** kwa ajili ya mishahara.

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA OFISI PEMBA

204. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Programu Ndogo ya uratibu wa Kazi za Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Pemba imepanga kuratibu shughuli za ufuatiliaji na tathmini wa miradi ya maendeleo ya Wizara; kuendesha vikao vya kupitia ripoti za utekelezaji kuratibu mipango ya Afisi, programu na sera

zinazotekelezwa; kuratibu na kufanya ufuatiliaji wa shughuli za Jumuiya Zisizo za Kiserikali (NGOs)*;* Kuimarisha shughuli za uratibu wa majukumu ya Wizara na kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa watumishi na kulipa stahiki zao kwa mujibu wa sheria pamoja na kuimarisha mahusiano ya Wizara na wadau wengine kwa upande wa Pemba.

205. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya uratibu wa Kazi za Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Pemba iIi iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 1,602,408,119** kati ya hizo **Shilingi 1,214,537,994** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 387,870,125** kwa ajili ya mishahara.

**PROGRAM NDOGO YA USAJILI NA URATIBU WA JUMUIYA ZISIZO ZA KISERIKALI**

206. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu na Usajili wa Jumuiya Zisizo za Kiserikali (NGOs) kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kufanya ufuatiliaji na ukaguzi kwa lengo la kutambua uhai wa Jumuiya hizo pamoja na kupima kiwango cha utekelezaji wa sheria, ahadi zao katika kukuza ustawi wa jamii, na utendaji katika kushughulikia kero katika jamii. Aidha, Afisi itafanya ziara za ufuatiliaji kwa Miradi ya maendeleo ya NGOs Unguja na Pemba na kukamilisha mapitio ya Sheria namba 6 ya mwaka 1995 ya Jumuiya zisizo za Kiserikali NGOs kwa lengo la kupunguza kero na usumbufu kwa wadau wa NGOs.

207. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Jumuiya zisizo za Kiserikali iIi iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 223,107,000 kwa matumizi mengineyo.

**WAKALA WA ULINZI JKU**

208. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala wa Ulinzi JKU imepanga kuendeleza ujenzi wa Mahanga maalum ya askari wa Wakala wa Ulinzi JKU Mtoni, kuimarisha doria kwa kununua gari na pikipiki tano (5), kuimarisha huduma za Utawala na Uendeshaji wa Wakala na kuimarisha mfumo wa mapato ya Wakala.

**209. Mheshimiwa Spika,** ili Wakala wa Ulinzi JKU iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 unaliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya Shilingi 653,300,000. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha mapato ya shillingi 1,750,000,000 kuchangia mfuko mkuu wa hazina.

**PROGRAMU KUU YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**210. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Idara ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepanga kutoa miongozo na Kanuni za uendeshaji wa Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa, na kutoa semina elekezi kwa viongozi wa Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa juu ya sera, sheria na kanuni za uendeshaji wa Mamlaka hizo pamoja nakuimarisha mahusiano baina ya Serikali kuu na Serikali za Mitaa.

**211. Mheshimiwa Spika,** iIi Programu ndogo ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 626,349,330 Kati ya hizo 383,275,000 kwa matumizi mengineyo, na Shilingi 243,074,330 kwa ajili ya mishahara.

**PROGRAMU KUU YA URATIBU NA USIMAMIZI WA IDARA MAALUM ZA SMZ**

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA IDARA MAALUM**

**212. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu Idara Maalum za SMZ imepanga kuimarisha maendeleo ya viwanda vya ushoni na viatu vya Idara Maalum, kuimarisha ukaguzi wa ndani wa hesabu za Taasisi za Idara Maalum za SMZ, kusimamia operesheni za Mji Salama, na kuimarisha mashirikiano baina ya vyombo vya ulinzi vya SMZ na SMT.

**213. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ili Programu ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ iweze kutekeleza majukumu yake inaomba iidhinishiwe jumla ya **Shilingi 18,508,267,500**. Kati ya hizo **Shilingi 607,289,500** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 17,900,978,000** kwa kazi za maendeleo ambapo Mradi wa Zanzibar Salama umepangiwa **Shilingi 12,000,000,000** na Mradi wa Viwanda vya Ushoni na Viatu vya Idara Maalum za SMZ **Shilingi 5,900,978,000**.

**TUME YA UTUMISHI WA IDARA MAALUM ZA SMZ**

**214. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Tume ya Utumishi Idara Maalum za SMZ imepanga kuimarisha masuala ya kiutumishi ikiwemo ajira, upandishaji wa vyeo pamoja na kupokea na kusikiliza malalamiko ya watumishi wa Idara Maalum za SMZ.

**215. Mheshimiwa Spika,** ili Tume ya Utumishi Idara Maalum za SMZ iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 inaliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya **Shilingi 207,500,000** kwa matumizi mengineyo.

**216. Mheshimiwa Spika,** ili programu zilizo chini ya Fungu D01 ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 25,862,078,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,792,606,000** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 5,307,694,000** kwa matumizi mengineyo, **Shilingi 860,800,000** kwa ajili ya ruzuku ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum na Wakala wa Ulinzi JKU na **Shilingi 17,900,978,000** kwa kazi za maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makusanyo ya mapato

**Shilingi 1,750,000,000** kwa Wakala wa Ulinzi JKU kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina.

**PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ - FUNGU (D02-D06)**

217. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Idara Maalum za SMZ zimetekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu 10 ambapo kila Fungu limetekeleza program kuu mbili. Maelezo yafuatayo yanahusu utekelezaji wa Programu hizo kuanzia Fungu D02 hadi D06.

**JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) - FUNGU D02**

218. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Jeshi la Kujenga Uchumi kupitia Programu ya Mafunzo kwa vijana, Uzalishaji Mali, Utawala na uendeshaji wa JKU limepanga kutekeleza shughuli za kuimarisha mafunzo ya amali na uzalendo kwa vijana, ili vijana waweze kujiajiri wanapomaliza mafunzo yao kwa lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuongeza ajira kwa vijana; kuimarisha shughuli za uzalishaji mali kwa kuekeza kwenye mradi wa kilimo cha umwagiliji katika bonde la JKU Msaani; kuimiarisha ufugaji wa kisasa kwa lengo la kuongeza uzalisha wa mifugo; kuimarisha shughuli za uvuvi zinazoendana na lengo la Serikali la kujenga uchumi wa buluu; kuendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Mahanga, nyumba za askari kwa kuweka mazingira bora ya maafisa, askari na vijana, kuimarisha uwezo wa Skuli ya Ufundi JKU Mtoni na Sekondari kuwa za daraja la juu kwa kuchukuwa wanafunzi wengi zaidi na kuvutia vijana wengi kujiunga na shule; na kuimarisha huduma za Utawala na uendeshaji wa JKU.

219. **Mheshimiwa Spika,** ili Jeshi la Kujenga Uchumi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 liweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 37,474,723,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 24,016,100,000** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 2,644,000,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 10,814,623,000** kwa kazi za maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makusanyo ya **Shilingi 105,000,000** kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

**CHUO CHA MAFUNZO - FUNGU D03**

**220. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2021/2022 Chuo cha Mafunzo kimepanga kuimarisha huduma za urekebishaji tabia kwa wanafunzi kwa kuwapatia mafunzo walimu wanaofundisha fani ya urekebishaji; kuimarisha shughuli za uzalishaji ili kupunguza utegemezi wa fedha za chakula cha wanafunzi na askari kutoka Serikalini; Kuimarisha mitaala ya mafunzo ya urekebishaji tabia ili kupunguza wimbi la wanafunzi kurejea tena chuoni baada ya kuwa huru kuimarisha; utoaji wa mafunzo kwa wapiganaji na maafisa ili kuwajengea uwezo kiutendaji; kuimarisha makaazi na mazingira bora ya kazi kupitia mradi wa ujenzi wa nyumba, mahanga na ofisi; kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa chuo cha mafunzo Hanyegwa Mchana ili kikidhi vigezo vya Kimataifa ikiwa ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa ilani ya CCM (2020-2025).

**221. Mheshimiwa Spika,** ili Chuo cha Mafunzo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kiweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 22,498,450,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 16,415,600,000** ni mishahara, **Shilingi 2,850,200,000** kwa ajili ya matumizi ya mengineyo na **Shilingi 3,232,650,000** kwa ajili ya kazi za maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makusanyo ya **Shilingi 94,400,000** kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

**KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) - FUNGU D04**

**222. Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ya Utawala na Uendeshaji, Kikosi Malum cha Kuzuia Magendokitatoa huduma za kuweka mazingira mazuri ya kuimarisha ulinzi na usalama wa Zanzibar kwa kudhibiti aina zote za magendo; kuimarisha huduma za uzamiaji na uokozi ili kwenda sambamba na uchumi wa buluu; kuimarisha huduma za afya katika hospitali ya KMKM Kibweni kwa kutoa huduma kwa wapiganaji na wananchi ; kuanza ujenzi wa chelezo Makao Makuu KMKM kwa lengo la kuhifadhi boti za KMKM na kupunguza gharama kwa serikali kupeleka vyombo vyake Mombasa Kenya; kuimarisha makaazi na mazingira mazuri ya kazi kwa maafisa na wapiganaji wa KMKM kupitia mradi wa ujenzi na ukarabati wa

mahanga, nyumba na majengo ya ofisi; kutoa stahiki za maafisa na wapiganaji kwa wakati.

**223. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kikosi kinaendelea na mradi wa ujenzi wa Mahanga ambao utajumuisha ujenzi wa jengo la utawala Wete Pemba, ujenzi wa Kambi ya Gando, Kibwengo na Unguja Ukuu kwa upande wa Unguja pamoja na kuendelea na mradi wa ujenzi wa chelezo Makao Makuu Kibweni.

**224. Mheshimiwa Spika,** ili Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kiweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisikwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 95,516,164,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 23,864,400,000** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 5,195,400,000** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 66,456,364,000** kwa miradi ya maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makusanyo ya **Shilingi 83,400,000** kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina.

**KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) - FUNGU D05**

**225. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kikosi kitaendelea kutekeleza programu kuu mbili ambazo ni programu ya uokozi na uzimaji moto na programu ya utawala na uendeshaji wa Kikosi. Kupitia programu ya uokozi na uzimaji motokwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kikosi kimepanga kuimarisha huduma za zimamoto na uokozi katika viwanja vya ndege na bandari kwa kuwajengea uwezo maafisa na askari wa maeneo hayo. Aidha, kupitia programu ya utawala na uendeshaji Kikosi kimepanga kuwapatia maafisa na askari haki zao kwa mujibu wa sheria, pamoja na kutoa mafunzo ya kiutendaji na kitaaluma kwa maafisa na wapiganaji.

**226. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa maendeleo, Kikosi kitaendelea na mradi wa ujenzi wa vituo, mahanga na nyumba kwa kujenga Kituo cha Zimamoto na Uokozi na Mahanga mawili Wete, kujenga mahanga mawili, Afisi ya zoni na ukarabati wa nyumba tatu katika kambi ya Mahonda, ujenzi wa Kituo kipya cha Zimamoto na Uokozi na hanga moja Kiwengwa, kujenga mahanga mawili katika kambi ya Kijichame, kujenga jengo la

utawala na kufanya ukarabati wa jengo la Afisi Kuu Chanjaani Chake Chake, pamoja na kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Chuo cha Zimamoto Kitogani.

**227.** **Mheshimiwa Spika,** ili Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kiweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisikwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe **Shilingi 19,172,000,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 11,606,400,000** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 2,358,700,000** matumizi mengineyo na **Shillingi 5,206,900,000** kwa kazi za maendeleo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makusanyo ya **Shilingi 79,838,000** kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina.

**KIKOSI CHA VALANTIA ZANZIBAR (KVZ) – FUNGU D06**

**228.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kikosi cha Valantia kitaendelea kutekeleza programu kuu mbili ambazo ni programu ya ulinzi wa nchi, raia na mali zao na programu ya utawala na uendeshaji wa Kikosi. Kupitia programu ya ulinzi wa nchi, raia na mali zao, Kikosi kimepanga kuimarisha huduma za ulinzi kwa kuendeleza doria za kawaida na doria maalum; kuwafikisha wapiganaji katika vituo vya ulinzi kwa wakati na kuwajengea uwezo maafisa na wapiganaji kwa kuwapatia mafunzo na vifaa vya kisasa vya ulinzi; na kununua sare kwa askari maalum waliofunzwa kutoa ulinzi wa viongozi waandamizi wa Serikali.

**229.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ya utawala na uendeshaji, Kikosi kimepanga kuimarisha mazingira mazuri ya kazi ikiwemo kufanya manunuzi ya basi kwa kusafirishia maafisa na wapiganaji; kulipa stahiki za maafisa na wapiganaji kwa mujibu wa sheria; kununua thamani na vifaa vya ofisini, kuimarisha huduma za afya katika kambi. Aidha, Kikosi kitaanza kufanya kazi za uzalishaji mali kwa kukamilisha ujenzi wa boti ya uvuvi na ununuzi wa vifaa vyake; kukamilisha matayarisho ya kilimo cha kisasa cha vitalu nyumba katika kambi ya Pujini na kuanza ujenzi wa Bekari ya kisasa katika Kambi ya Mtoni.

**230.** **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji miradi wa maendeleo, Kikosi kitaendeleza na mradi wa ujenzi wa ofisi, nyumba na mahanga ambapo majengo hayo yatajengwa katika kambi za Pujini, Muyuni, Mto wa

Maji, Kisakasaka, Mwanyanya pamoja na kufanya ukarabati wa majengo Kambi ya Pangatupu na ukuta wa Makao Makuu Mtoni.

231. **Mheshimiwa Spika,** ili Kikosi cha Valantia kiweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisikwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 22,678,100,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,905,000,000** kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 2,603,100,000** matumizi mengineyo na **Shilingi 4,170,000,000** kwa miradi ya maendeleo.

**KAMPUNI YA UJENZI YA SERIKALI**

232. **Mheshimiwa mwenyekiti,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kampuni ya Ujenzi ya Serikali imepanga kuimarisha ukushanyaji wa mapato yake kupitia kazi zake za ujenzi, kuwajengea uwezo wafanyakazi wake, kukuza tasnia ya ujenzi nchini kwa kujenga majengo bora na kwa gharama nafuu pamoja na kutoa fursa za mafunzo kwa njia ya vitendo kwa mafundi wazalendo na kuchangia katika kuimarisha uchumi wa buluu kwa kushiriki katika ujenzi wa miundombinu mbali mbali.

233. **Mheshimiwa mwenyekiti**, kwa vile Kampuni ya Ujenzi ya Serikali ni mpya na haina mtaji, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kampuni inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,547,100,000** ikiwa ni sehemu ya mtaji. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,446,650,000** sawa na asilimia **94** ni kwa ajili ya ununuzi wa mashine na vifaa vya ujenzi na vya afisi, **Shilingi 100,450,000** sawa na asilimia **6** ni kwa ajili ya uendeshaji wa afisi. Gharama nyengine zote za kuendeshea Kampuni zitatoka katika vyanzo vya mapato ya ndani ya Kampuni. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kampuni ya Ujenzi ya Serikali inatarajia kupata Kandarasi zenye thamani ya **Shilingi 22,080,000,000** na kutengeneza faida ya **Shilingi 2,500,000,000**.

**PROGRAMU ZA TAWALA ZA MIKOA - FUNGU (D07-D11)**

234. **Mheshimiwa Spika,** Mikoa yote imepanga shughuli zake chini ya Programu Kuu tatu ambazo ni Programu ya Kusimamia Shughuli za Serikali katika Mkoa; Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa Tawala za Mikoa; na Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Maelezo yafuatayo yanahusu mwelekeo wa utekelezaji wa Programu za Tawala za Mkoa kwa kila Fungu kuanzia fungu D07-D11.

**MKOA WA MJINI MAGHARIBI – FUNGU D07**

**235. Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu ya Usimamizi wa Shughuli za Serikali Mkoa wa Mjini Magharibi umepanga kuimarisha masuala ya ulinzi na usalama; kudhibiti wizi wa mazao, rasilimali ya mchanga na mifugo katika Wilaya za Magharibi 'A' na Magharibi 'B'; kuimarisha maendeleo ya elimu; kupunguza wimbi la migogoro ya ardhi; kufuatilia ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kupunguza vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake, watoto na unyanyasaji wa kijinsia pamoja na kupunguza tatizo la ajira kwa vijana kwa kuwaelimisha kutochagua kazi za kufanya.

**236. Mheshimiwa Spika,** Mkoa kupitia programu ya Utawala na Uendeshaji imepangiwa kuyapatia ufumbuzi malalamiko ya wananchi, kuimarisha mazingira ya kazi na kuwapatia stahiki watumishi pamoja na kuweka mfumo wa kidigitali katika uendeshaji wa kazi za Mkoa.

**JIJI LA ZANZIBAR**

**237. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kupitia programu ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa, Jiji la Zanzibar limepanga kuandaa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Jiji; kuandaa maandiko ya miradi ya usafiri wa umma na uwekaji wa mabango na matangazo ya biashara kwa njia ya kielektroniki.

**BARAZA LA MANISPAA MJINI**

**238. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Baraza la Manispaa Mjini limepanga kuimarisha usafi wa mazingira, kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa njia za kielektroniki na kutenga maeneo maalum ya kudumu kwa ajili ya wafanya biashara wadogo wadogo.

**BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI 'A'**

**239. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Baraza la Manispaa Magharibi 'A' limepanga kuimarisha huduma na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi ikiwemo ujenzi wa soko dogo Mtopepo, kuimarisha usafi wa mazingira kwa ujenzi wa silabi tatu katika Shehia za Mtopepo, Kikaangoni na Mwanyanya, kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kufanya matengenezo ya mifumo ya utoaji huduma.

**BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI 'B'**

**240. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Manispaa Maghribi 'B' limepanga kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa njia za kielektroniki, kuimarisha usafi wa mazingira na kuweka bustani, kuwawekea maeneo maalum na ya kudumu Wafanyabiashara wadogo wadogo pamoja na kuimarisha huduma za kijamii kupitia Miradi ya maendeleo inayoibuliwa na Kamati za Mashauriano za Shehia.

**241. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ili Mkoa wa Mjini Magharibi uweze kutekeleza programu zake naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 10,965,400,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 7,849,800,000** ni ruzuku ya Jiji na Mabaraza ya Manispaa, **Shilingi 1,800,800,000** ni mishahara ya Afisi ya Mkuu wa Mkoa na **Shilingi 1,314,800,000** ni matumizi mengineyo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe mapato ya **Shilingi 148,700,000** ili kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina. Vile vile, naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makusanyo ya mapato ya ndani ya Baraza la Manispaa ya Mjini **Shilingi 5,252,940,000**, Baraza la Manispaa ya Magharibi 'A', **Shilingi 1,200,000,000** na Baraza la Manispaa Magharibi 'B' **Shilingi 2,200,000,000**.

**MKOA WA KUSINI UNGUJA – FUNGU D08**

242. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mkoa wa Kusini Unguja, kupitia Programu ya Kusimamia Shughuli za Serikali katika Mkoa, Wilaya na Shehia umepanga kusimamia shughuli za usalama; Kufuatilia utekelezaji wa shughuli za sekta katika Mkoa, Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto; Kutatua malalamiko, kero za wananchi na migogoro ya ardhi, Kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyomo ndani ya Mkoa na Kuendeleza Kamati ya Takwimu ya Mkoa. Aidha, Mkoa umepanga kuendeleza Dawati la kupambana na Vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi, Kuimarisha maendeleo ya elimu; Kupiga vita wizi wa mifugo na mazao ya wafugaji na wakulima na Kutoa mafunzo ya uibuaji wa miradi kwa vijana.

243. **Mheshimiwa Spika,** katika Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Mkoa, Wilaya na Shehia, Mkoa umepanga kuzipatia Afisi huduma za Utawala na Uendeshaji ikiwemo kuwapatia wafanyakazi stahiki zao pamoja na kutoa msaada wa kitaalamu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

**BARAZA LA MJI KATI**

244. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu ya Usimamizi wa Serikali za Mitaa, Baraza la Mji Kati kwa mwaka 2021/22 limepanga kuimarisha na kuongeza wigo na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na utoaji wa huduma kwa jamii, usafi wa mazingira, kuweka mazingira bora ya kazi, kuyajengea uwezo mabaraza ya wadi na kamati za mashauriano za shehia, ujenzi wa masoko madogo madogo katika maeneo 11 ya Wilaya ambayo ni; Dunga Kiembeni, Dunga Mitini, Mwera, Mchangani, Kikungwi, Jozani, Jumbi Kilimani, Unguja Ukuu Kaepwani, Cheju, Hanyegwa Mchana na Ndijani kwa Baniani, ufugaji wa nyuki katika maeneo ya Cheju, Dunga na Uzi, mradi wa Usafi wa mazingira, na kuwajengea uwezo wajasiriamali yakiwemo makundi maalumu.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI**

**245. Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kwa mwaka fedha 2021/2022, imepanga kuongeza ukusanyaji wa mapato; kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo ya Miji, fukwe, na maeneo ya utalii; Uwezeshaji wa makundi maalum ya kijamii; ununuzi wa gari ya kuzolea taka pamoja na vifaa vya usafi; kuimarisha maegesho ya magari; kuwawekea mazingira mazuri wajasiriamali na kutoa huduma za utawala na uendeshaji wa Afisi pamoja na kuendeleza Mabaraza ya Wadi na Kamati za Mashauriano za Shehia.

**246. Mheshimiwa Spika,** ili Mkoa wa Kusini Unguja uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe **Shilingi 4,043,000,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,639,500,000** kwa matumizi ya mishahara, **Shilingi 581,000,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 1,822,500,000** ni ruzuku za mishahara kwa Baraza la Mji Kati na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha **Shilingi 74,332,000** kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Kwa upande wa makusanyo ya ndani, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha **Shilingi 1,500,000,000** kwa Baraza la Mji Kati na **Shilingi 700,305,000** kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini.

**MKOA WA KASKAZINI UNGUJA – FUNGU D09**

**247. Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na Mabaraza ya Miji ya Kaskazini "A" na Kaskazini "B" kwa mwaka wa fedha 2021/2022 utatekeleza programu kuu tatu ambazo ni; Programu ya kusimamia shughuli za Serikali katika Mkoa, imepanga kuimarisha shughuli za ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kusimamia miradi ya maendeleo, kuratibu shughuli za uwekezaji wa kiuchumi katika sekta za utalii, viwanda na biashara. Kusimamia na kuratibu maendeleo katika Serikali za mitaa. Aidha, katika kutekeleza azma ya Serikali ya awamu ya nane chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Mkoa umepanga kuratibu na kusimamia maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi ya bandari, barabara na uwanja wa ndege na kuanzisha miji mipya ya Mangapwani, Mahonda, Mkokotoni na ukanda wa pwani ya mashariki wa

Matemwe - Pwani Mchangani – Kiwengwa ambapo hatua za awali za utayarishaji wa mpango mkuu wa Mkoa (master plan) zimeanza.

**248. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Mkoa, imepanga kuyaunganisha makundi mbalimbali katika jamii kama vile vijana, wazee, wanawake na watoto katika kushiriki na kujitolea kwa lengo la kusaidia maendeleo ya Mkoa pamoja na kuzipatia huduma za utawala na uendeshaji ofisi. Kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa kusimamia ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya, ukarabati mkubwa wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na kusimamia maslahi na stahiki za wafanyakazi.

**BARAZA LA MJI KASKAZINI 'A'**

**249. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa. Baraza la Mji Kaskazini 'A' limepanga kuimarisha utowaji wa huduma za kijamii,ukusanyaji na udhibiti wa mapato kwa njia ya kielectronik, Kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo yote, kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika jamii, kuimarisha mazingira ya kutendea kazi pamoja na kukuza utawala bora.

**BARAZA LA MJI KASKAZINI 'B'**

**250. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Baraza la Mji Kaskazini 'B' limepanga kuimarisha huduma za kijamii na uzalishaji, ukusanyaji wa mapato; Kuimarisha usafi wa mazingira, Kutekeleza miradi ya wananchi itakayoibuliwa kupitia mabaraza ya Wadi na Kamati za mashauriano ya Shehia; kuwasajili wajasiriamali wote na kuwapatia vitambulisho pamoja Kuwawekea mazingira wezeshi.

**251. Mheshimiwa Spika,** ili Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mwaka wa fedha 2021/2022 uweze kutekeleza programu zake kwa ufanisi naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,284,800,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,520,700,000** ni mishahara, **Shilingi 824,700,000** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 1,939,400,000** ni kwa ajili ya ruzuka ya Mabaraza ya Miji kaskazini 'A' na 'B'. Vile vile, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe makusanyo ya mapato ya **Shilingi 61,360,000** kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Kwa upande wa makusanyo ya mapato ya ndani,

naomba kuidhinishiwa Baraza la Mji Kaskazini "A" kukusanya **Shilingi 1,414,483,450** na Baraza la Mji Kaskazini 'B' kukusanya **Shilingi 1,609,555,898**.

**MKOA WA KUSINI PEMBA – FUNGU D10**

**252.** **Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Kusini Pemba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 umepanga kusimamia Ulinzi na Usalama, kusimamia upatikanaji wa huduma bora za jamii, kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa kupiga vita udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto, mapambano dhidi ya dawa za kulevya, wizi wa mazao, kuratibu sherehe za Kitaifa na ziara za Viongozi, kusimamia na kufuatilia maendeleo ya zao la karafuu, kusimamia Utalii na biashara na kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE**

**253.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Baraza limepanga kuimarisha ukusanyaji na udhibiti wa mapato kwa njia ya kielektroniki, kuimarisha mazingira ya kuiutendaji, kuimarisha usafi wa mazingira katika eneo la Mji, kuimarisha huduma za maendeleo kwa kuanza utayarishaji na ujenzi wa eneo la huduma kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na kuimarisha uratibu wa masuala mtambuka na kuunga mkono miradi ya maendeleo inayoibuliwa na wananchi.

**BARAZA LA MJI MKOANI**

**254.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Baraza limepanga kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki, kuimarisha mazingira ya kiutendaji, kutekeleza miradi ya ujenzi wa njia za vidaraja, kufanya matayarisho ya awali ya ujenzi wa soko la Mtambile na Kengeja, kufanya ukarabati wa chinjio na soko la Samaki na matunda Mbuyuni na uendelezaji wa Shamba la Bustani Mtuhaliwa na kuunga mkono miradi ya maendeleo inayoibuliwa na wananchi.

**255.** **Mheshimiwa Spika,** ili Mkoa wa Kusini Pemba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 uweze kutekeleza programu zake kwa ufanisi naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 4,937,600,000**. Kati ya fedha

hizo **Shilingi 1,404,700,000** ni mishahara, **Shilingi 738,100,000** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 2,794,800,000** ni ruzuku ya Baraza la Mji Chake Chake na Baraza la Mji Mkoani. Naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe makusanyo ya **Shilingi 63,320,000** na kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina. Aidha, naliomba Baraza lako liidhinishe makusanyo ya mapato ya ndani **Shilingi 655,000,000** kwa Baraza la Mji Chake na **Shilingi 460,000,000** kwa Baraza la Mji Mkoani.

**MKOA WA KASKAZINI PEMBA – FUNGU D11**

**256. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mkoa wa Kaskazini Pemba umepanga kusimamia na kudumisha Amani nausalama; kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mkoa; Kuandaa utafiti wa awali juu ya udhalilishajiwa Kijinsia katika Mkoa; Kuratibu Misaada ya Kijamii kwa wananchi wenye mazingira magumu; Kusimamia Maendeleo ya biashara na wajasiriamali wadogo wadogo, uzalishaji wa mazao ya Chakula na Biashara; Kusikiliza na kufuatilia kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi; kuwawekea watumishi mazingira mazuri ya kufanyia kazina kusimamia utekelezaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**BARAZA LA MJI WETE**

**257. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Baraza la Mji Wete limepanga kutekeleza mambo yafuatayo:- kufanya ujenzi wa bustani katika eneo la holi la Jamhuri; kufanya ukarabati wa ukumbi wa holi la Jamhuri; kujenga silabi za kukusanyia taka; kuwajengea wajasiriamali sehemu maalum za kufanyia biashara ikiwemo ukarabati wa masoko pamoja na kuyawezesha makundi maalumu ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kuwapatia mikopo nafuu; kuongeza nguvu katika upanuzi wa wigo wa kodi na kuongeza ukusanyaji wa mapato; kuwapatia watumishi stahiki zao kwa mujibu wa sharia ikiwemo kuwajengea uwezo; kutoa misaada kwa wananchi walioathirika na maafa na majanga mbali mbali na kuendeleza usafi wa Mazingira katika Mji kwa ajili ya afya na kuvutia wageni na kujenga maeneo ya maegesho kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI**

**258. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:- kuandaa na kutekeleza miradi ya Maendeleo kwa wananchi wa Wilaya ya Micheweni; kuendeleza usafi wa Mazingira katika Mji; kuongeza nguvu katika upanuzi wa wigo wa kodi na kuongeza ukusanyaji wa mapato; kuweka mazingira mazuri kwa watumishi ikiwa ni pamoja na maandalizi ya ujenzi wa Afisi; kuwapatia watumishi stahiki zao; kuwajengea wajasiriamali sehemu maalum za kufanyia biashara pamoja na kuyawezesha makundi maalumu ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kuwapatia mikopo nafuu na kuendeleza maeneo ya maegesho Konde kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

**259. Mheshimiwa Spika,** ili Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa mwaka wa fedha 2021/2022 uweze kutekeleza programu zake kwa ufanisi naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 5,198,300,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,244,400,000** ni mishahara, **Shilingi 758,100,000** kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 3,195,800,000** ni ruzuku ya Baraza la Wete na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe makusanyo ya Mkoa **Shilingi 59,135,000** kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina. Aidha, naomba kuidhinishiwa makusanyo ya mapato ya ndani kwa Baraza la Mji Wete **Shilingi 413,050,000** na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni **Shilingi 370,000,000**.

**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII –FUNGU D12**

**260. MheshimiwaSpika,**kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijaamii imepanga kuimarisha Mfumo wa Vitambulisho kwa ajili ya Wafanyakazi wa Taasisi mbalimbali za umma na binafsi (*Multi-Id System*), Kununua Mali ghafi za Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, Vitambulisho vya Mfumo wa *Multi-Id* pamoja na Vitambulisho vya Wakaazi wasiokuwa Wazanzibari, kununua Malighafi zote zinazohitajika kwa ajili ya Usajili wa Vizazi hai na Vifo, Ndoa na Talaka pamoja na Magamba yanayotumika kutengeneza Vyeti vya Matukio hayo.

Aidha Wakala imepanga kuanza Kuutumia Mfumo wa Usajili wa wakaazi wasiokuwa Wazanzibari baada ya kukamilika.

